# Upendo Katika Ukristo Na Uislamu

# Upendo Katika Ukristo Na Uislamu



Mahnaz Heydarpoor

Kimetafsiriwa na
Dr. M. S. Kanju

Al-Islam.org

### Author(s):

Mahnaz Heydarpoor [1]

### Publisher(s):

Al Itrah Foundation [2]

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza, kwa jina la: “Love in Christianity and Islam.” Sisi tumekiita: “Upendo katika Ukirsto na Uislamu. Kitabu hiki, “Upendo katika Ukristo na Uislamu” ni matokea ya utafiti wa kielimu uliofanyika na Mwanachuoni wa Kiislamu, Bi. Mahnaz Heydarpoor.

Get PDF [3] Get EPUB [4] Get MOBI [5]

### Translator(s):

Dr. M. S. Kanju [6]

### Topic Tags:

Love [7]
Christianity [8]
Islam [9]
History [10]

### Person Tags:

Prophet Muhammad [11]
Prophet Moses [12]
Imam Ja'far al-Sadiq [13]

# Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza, kwa jina la: ***“Love in Christianity and Islam.”*** Sisi tumekiita: “**Upendo katika Ukirsto na Uislamu**.”

Kitabu hiki, “**Upendo katika Ukristo na Uislamu**” ni matokea ya utafiti wa kielimu uliofanyika na Mwanachuoni wa Kiislamu, **Bi. Mahnaz Heydarpoor**.

Bi. Mahnaz Heydarpoor ni mke wa mwanachuoni mkubwa wa Kiislamu, Sheikh Dr. Mohamed Shomali. Bi. Mahnaz ni mhitimu wa chuo Kikuu mashuhuri cha Qum, Iran. Alikwenda Uingereza kuungana na Mumewe ambaye alikwenda huko kwa ajili ya masomo. Kwa vile na yeye ni msomi aliona asikae bure bali aitumie fursa hiyo kufanya utafiti wa upendo katika Ukiristo na Uislamu, ili kuona dini hizi kubwa mbili zinazungumzia nini kuhusu nukta hiyo na mchango wao katika maadili na uadilifu.

Ili kufanikiwa katika utafiti wake alifanya mazungumzo ya mara kwa mara na Wakristo, kuishi nao katika vyuo vyao vya kidini na kuhudhuria mikutano yao. Matokeo ya shughuli hiyo yote ni kitabu hiki ulichonacho mikononi mwako.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya '**Al-Itrah Foundation**' imeona ikitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yale yale ya kuwahudumia

Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili. Tunamshukuru ndugu yetu, **Dr. M. S. Kanju** kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation**
**S. L. P. 19701**
**Dar-es-Salaam.**

# Dibaji

Maudhui iliyoshughulikiwa katika kitabu hiki ni ya umuhimu mkubwa sana. Inataka kuonesha vipi upendo ulivyo katika moyo wa kiroho na maadili ya imani mbili kubwa, kati kati yake ambapo kujuana kukubwa na kufahamiana baina ya imani hizi mbili kunahitajika kwa haraka mno iwezekanavyo.

Uhusiano kati ya Wakristo na Waislamu umepatwa na athari ya urithi wa historia wa mashaka na chuki inayojitokeza katika nyakati ambapo falme zenye nguvu na ustaarabu ulioshirikishwa nazo, wamejikuta wenyewe katika mizozo na mapambano. Ushindi wa Waislamu wa rasi ya Iberia, vita vya msalaba, kuanguka kwa Constantinople, nia ya ukubwa wa dola ya Ottoman na ubeberu wa magharibi wa karne ya 19 na ya 20, yote haya yameacha mabaki ya machungu na uadui.

Hii imeendelea leo kujidhihirisha yenyewe katika Mashariki ya Kati, katika Balkan na katika sehemu mbali mbali za ulimwengu. Katika jamii za magharibi taarifa za vyombo vya habari juu ya harakati za vurugu za Waislamu wanaowaita wa siasa kali au imani kali vimeelekea pasina haki kabisa, kuhusisha

Uislamu na Waislamu na ushabiki wa dini ambao kwa kiasi kikubwa umeondolewa katika upendo. Ni kana kwamba ule uhusiano kati ya Wakatoliki na Waprotestanti katika Northern Ireland ni wa kuwakilisha uhalisi wa Ukiristo.

Pamoja na mambo haya ya kusikitisha, kuna vipengele zaidi mno vya historia ambavyo ni bayana vya uhusiano kati ya imani hizi mbili na ustaarabu wao. Ni rahisi mno kusahau miundo mingi ya elimu ya wote pamoja na utajiri wa utamaduni walioshirikiana katika sanaa, usanifu majengo, filosofia, hisabati, sayansi, na fasihi kwa karne nyingi.

Maeneo ya mapatano ya kiteolojia kati yao (na vile vile na uyahudi), yamekuwa vile vile yanafahamika kwa kiasi kidogo sana. Wana kukubaliana kwa sawa sawa kuhusu ufunuo wa vitabu vya dini na simulizi za kiutume za imani hizi mbili; uthibitisho wa pamoja wa imani katika Mungu wa Ibrahim; na msisitizo mkali juu ya umuhimu wa kumtukuza Mungu katika ibada na kuishi maisha katika njia iliyoelekezwa na sheria Zake.

Kufanana na mwingiliano wa fikra na kiroho wa baadhi ya walimu wakubwa na mairifani wakati wa kipindi cha karne za kati huonekana vile vile kusahauliwa kabisa.

Hata hivyo, katika kubadilisha maadili ya kijamii ya mfumo wa misimamo mingi zaidi ya kidini, hali ya uungaji mkono ya ukoloni katika nchi za magharibi, na hisia kubwa ya jumuiya ya ulimengu mzima (utandawazi) iliyoletwa na mawasiliano bora, kwa haraka misimamo inageuka. Mazungumzo kati ya imani za dini na utashi wa kutafuta ujuzi wa kweli, kuachwa huru kutoka chapa za zamani na za kisasa, kumejitokeza zaidi mno katika nchi za magharibi, shukurani kwa kazi za wanachuoni kama vile John Esposito na Ninian Smart.

Ingawa kukua kwa jumuiya za Kiislamu katika jamii za watu wa Ulaya hakukuwa bila matatizo na migogoro, utashi mkubwa unajitokeza miongni mwa kizazi cha vijana ili kuweka hali ya baadaye ya pamoja iliyosimama juu ya kuheshimiana na kujifunza imani na utamaduni kutoka kwa kila mmojawao.

Ni kwa ajili ya moyo huu kwamba kitabu hiki kimeandikwa. Kwa mtazamo wa matatizo mazito ambayo yamejitokeza kati ya Iran, U.S.A na U.K. kwa miongo miwili iliyopita, haya yote ni ya muhimu zaidi kwamba kitabu hiki ni cha mwanachuo kijana, Shia wa Iran, Mahnaz Heydarpoor. Mhitimu wa Chuo Kikuu mashuhuri cha Qum, ambaye alikuja Uingereza na mumewe na familia yake katika mwaka wa 1997, mara tu alionesha kuvutiwa katika kuchukua mafunzo zaidi na utafiti. Imekuwa ni furaha kubwa kwangu kuwa msimamizi wake na kukutana na wote, Mahnaz na mumewe Mohammad Shomali, ambaye yeye mwenyewe ni mwanachuoni mwenye kuheshimika. Wote wamekuwa mabalozi wazuri kwa Iran na kwa Uislamu na nimejfunza mengi kutoka kwao kuhusu tabia na moyo wa Uislamu kisha kutokana na kusoma vitabu vingi.
Shauku ya Mahnaz ya kuamua kuongeza ujuzi wake wa Ukiristo na juhudi na nguvu ambazo kwazo amefuatilia lengo lake hili, sio tu kwa kusoma vitabu, bali pia kwa kukutana na Wakristo wa usuli za madhehebu mbali mbali na vikundi kama vile Chama cha Focolare, imekuwa ya kuvutia mno.

Uchanganuzi wake juu ya upendo katika Ukiristo ni wa kisomi na wa utambuzi mno, lakini itakuwa ni ufafanuzi wake wa ukuu wa upendo katika teolojia ya Kiislamu na maadili ambao hususan utakuwa wa kuvutia kwa wasomaji wa Magharibi, Wakristo na wengineo.

Inatumainiwa kwamba ari ya Mahnaz itaweza kulipwa na wasomi wengi, kama yeye wanaotafuta maeneo ya mazungumzo ili kuzidisha tathmini ya wote na ujuzi kati ya Uislamu na Ukiristo. Vile vile inatumainiwa kwamba ukunjufu na ukarimu wa kiroho (kwa neno, upendo wake) vile vile utalipwa, ili kwamba uponaji wa vidonda vya huzuni vilivyosababishwa na chuki ya karne nyingi na kutokuelewana kunaweza kuharakishwa kwa faida ya mamilioni.

**Dr. Dennis Bates, Manchester**
**Metropolitan University.**

# Utangulizi

***Kila moyo ambao hauwaki sio moyo;***
***Moyo ulioganda si chochote bali ni ukafi wa udongo wa mfinyazi.***
***Ewe Mungu! Nipe kifu ambacho kinawaka.***
***Na katika kifua hicho moyo, na moyo ule unaotafunwa na moto.***
(**Vashi Kermani, 1583**)

Ingawa inaweza kuonekana wazi kwa watu wengi kwamba hakuwezi kuwa na maadili bila kuwa na itikadi au imani katika Mungu, siku zote kumekuwa na mgogoro juu ya suala hili au kwa ujumla zaidi juu ya uhu- siano kati ya maadili na dini.

Miongoni mwa wanateolojia wote wa Kikristo na wa Kiislamu kumekuwepo na baadhi ya wanachuoni ambao wanaamini katika tegemezi kamilifu la maadili juu ya amri za mungu na ufunuo, kama ambavyo kuna wengine ambao wanaamini katika uhuru wa maadili. Kwa mujibu wa kwanza ‘haki ya kimaadili’ maana yake ‘imeamriwa na Mungu’ na ‘makosa ya kimaadili’ maana yake ‘yamekatazwa na Mungu.’

Msimamo wa upande mwingine hushikilia kwamba kuna kigezo tegemezi cha mema na mabaya ambacho huweza kueleweka katika akili zetu. Kwa hiyo kuna uwezekano wa kuwa na maadili tegemezi ya dini.

Hata hivyo, watu hawa kwa kawaida huchukulia kwamba dini inaweza kutoa maelezo ya wazi na mapana zaidi ya maadili. Makundi yote hukubaliana kwamba dini hutoa maadili pamoja na vizuizi. Kwa hiyo, mdahalo miongni mwa wanachuoni wa dini sio kwamba imma dini huchangia kwenye maadili au iwapo kuna kitu kama ‘maadili ya kidini’, bali ni juu ya upeo wa mchango huu.

Katika kitabu hiki nitajaribu kuelezea dhana ya maadili ya kidini na baadhi ya sifa zake na kisha nitalenga juu ya dhana ya upendo kwa kiini cha dhana katika maadili ya kidini. Kuna ushirikiano wa msimamo kwenye upendo miongoni mwa dini zote kubwa za ulimwenguni.

Hata hivyo, wakati mwingine inaeleweka katika njia tofauti ndani ya tamaduni tofauti. Katika sura ya pili na ya tatu nitajaribu kuchunguza umuhimu na misingi ya kiitikadi ya upendo katika dini mbili kubwa za ulimwenguni: Ukristo na Uislamu. Katika kila suala nitachunguza vipengele tofauti vya upendo wa Mungu (kwa Yeye Mwenyewe, kwa viumbe wote na kwa wanadamu) na upendo wa binadamu (kwa Mungu na kwa wanadamu wenzake).

Hapa lazima niseme kwamba kile ambacho kwa hakika nataka kukifanya ni kuchunguza Ukristo na Uislamu wa nyuma, yaani, katika maendeleo yao ya kihistoria, kwa sababu tunachohusika nacho hapa kwa hakika ni kuona, kwa mfano, mchango halisi wa dini hizi kwenye maadili. Kitu ambacho tutafanya ni kuhakikisha kwamba tuna ujuzi wa kuaminika wa kila dini kama ilivyo leo hii.

Ili kuelewa maadili ya Ukristo na Uislamu, utafiti wangu utahusisha baadhi ya tafsir za maandiko matukufu. Nimetegemea zaidi juu ya Bibilia na Qur'ani Tukufu sambamba na hadithi (simulizi za Mtume Muhammad) kama vyanzo vya mwanzo vya maadili ya Kikristo na Kiislamu, hususan wakati ninapojadili wajibu wa upendo katika dini zote. Nilichofanya katika kazi hii kimekuwa ni kugundua kijumla picha inayokubalika ya upendo katika dini mbili hizi. Vinginevyo labda itajwe, nimejaribu kurejea kwenye nukta za kawaida na kile kinachokubalika kwa wote Wakristo na Waislamu.

Hakika katika kanuni, kunaonekana kuwa na tofauti nyingi kati ya wanachuoni tofauti wa kila dini juu ya suala lililoko kwenye mjadala. Natambua kwamba tayari kumekuwa na tafiti nyingi juu ya vipengele tofauti, hususani kuhusu upendo katika Ukristo.

Hata hivyo, nafikri kwamba bado kuna haja ya kufanya utafiti kama huu uliokusudiwa hapa. Faida moja ya utafiti huu ni kwamba unachunguza suala hili kiulinganishi na sio tu katika dini moja. Faida ya pili, utafiti huu hujumisha mjadala kuhusu wajibu wa upendo katika maadili ya Kislamu, ambao huenda ukawa haujulikani kwa wasomaji wazungumzaji wa lugha ya Kiingereza. Faida ya tatu ni kwamba utafiti huu unatumia njia ya kuenda kwenye vyanzo vya asili vya Kiislamu katika lugha ya Kiarabu na Kifursi. Hivyo natumaini kwamba utafiti huu unaweza kutoa mchango wenye manufaa kwenye nyanja hii.

Hapa ningetaka kutamka kwamba suala la upendo limekuwa lenye kunishughulisha sana katika maisha yote ya ukubwani. Nilikuwa na umri wa miaka 16 tu wakati nilipopatwa na shauku kubwa mno kwa upendo wangu kwa ajili ya kumjua Mungu na kuwa karibu naye kiasi kwamba nilihisi nisingeweza kuendelea tena na maisha yangu ya kawaida. Pamoja na mipango yote ambayo wazazi wangu wamenipangia huko nyuma kwa ajili yangu, niliamua kabisa kuanza maisha mapya.

Pamoja na baraka za wazazi wangu niliondoka mjini kwangu na kwenda kwenye mji wa Qum, ambamo moja ya seminari kubwa ya Kiislamu imekuwepo humo kwa muda kwa zaidi ya miaka elfu moja. Nilijitolea maisha yangu katika kupanua ilmu yangu ya Uislamu, na la muhimu zaidi kujisogeza zaidi kwa

Mungu. Ingawa sifurahii mafanikio niliyopata nina imani kabisa kwamba nilifanya uamuzi ulio bora kwa ajili yangu, na nimechagua njia yenye mwanga zaidi, njia ya upendo.

Wakati wa utafiti kwa ajili ya kazi hii, sikusoma tu kuhusu nukta yangu, yaani upendo, bali vile vile nilijaribu kuishi kwa nukta yangu hii na kuishuhudia katika maisha ya wengine. Wakati huo (Julai 1999) nilikaa juma zima pamoja na baadhi ya marafiki wakristo huko Mariapolis mjini Windermere. Huko niliona mambo mengi ya kufanana kati ya Uislamu na Ukristo na jinsi upendo wa kweli kwa Mungu na wanadamu wenzako unavyoweza kuleta moyo mpya kwenye maisha, na maisha mapya kwenye jamii ya kisasa. Nilikumbushwa uzoefu wangu mweyewe wakati nilipoingia seminari ya Qum. Sasa nimewaona wengine ambao huamini kwayo na kufuata njia ile ilenjia ya upendo.

Kuanzia hapo nilifanya kila niwezalo kuendeleza ujuzi wangu wa ukristo, kama ulivyoanza, na kama unavyotekelezwa leo. Sio tu kwamba nime- fanya marafiki wengi binafsi, bali vilevile nilitembelea taasisi mbali mbali za kikristo na sehemu za ibada na elimu. Kwa mfano, mwezi oktoba 1999, nilialikwa kwenye mkutano juu ya Uislamu na Ukristo ulioandaliwa na *Focolare Movement* mjini Rome. Mbali na kuhudhuria mkutano, nilipata nafasi ya kuwa mzoefu zaidi na Vatican na Roman Catholic Church (kanisa Katoliki). Vilevile nilikaa siku chache mjini Loppiano, mji mdogo karibu na Florence.Wakazi wote wa mji huu hujaribu kutekeleza Focolare kiroho na hususan kumpenda Mungu na jirani yao. Kwa ujumla nilikaa siku kumi nchini Italia ambako vile vile nilipata nafasi ya kukutana na Chiara Lubich, mwasisi wa tasisi na baadhi ya masahaba wake wa mwanzo ambao walizungumzia kuhusu sala na upendo.

Mwezi Februari 2000, nilikaa siku mbili kwenye chuo cha Mt. Yohana (*St.John's college*) katika chuo kikuu cha Durham, kituo muhimu ndani ya kanisa la England kwa mafunzo ya uchungaji. Nilikutana na kuongea na Rt. Revd. Stephen Sykes, mkuu wa St. John's College na vile vile Mwenyekiti wa Kamisheni ya Mafundisho ya Kanisa la Uingereza (*Doctrine Commission of the church of England*), na pamoja na Dr. Croft, Dr. Wakefield na kundi la wanafunzi.

Mwezi Mei 2000, nilikaa juma zima huko Ampleforth Abbey ambako nilifanya vikao pamoja na Abbot na baadhi ya watawa wengine. Wakati wa vikao hivi, nilikujaelewa zaidi kuhusu Ukristo kiroho na asili ya maisha ya utawa. Lazima nitoe utajo maalum wa Cyprian Smith, mwandishi wa kitabu; *The way of Paradox: Spiritual Life as Taught by Meister Eckhart* na *The Path of Life*, ambaye kwa upole aliongea nami kuhusu mafunzo ya Ki-mungu ya Kikristo na ya kiroho, ya Benedictine order.

Vile vile nilinufaika kutokana na vitabu vya thamani vya maktaba ya watawa. Mwezi Juni 2000 nilikaa juma lingine huku Mariapolis, pamoja na mamia ya marafiki wakristo wa Katoliki na wa Angalikana kutoka Uingereza na sehemu nyingine za ulimwengu huko Stirling Seotland.

Nimejadili upendo katika Ukristo na marafiki wengi Wakristo, kama vile Dom Jonathan Cotton OSB, Leyland, Canon Simor Hoare, Skipton, Dimitrij Bregant, Rome na Dom Wulstan Peterburs OSB, Ampleforth. Watatu wa mwisho walisoma mswada wa sura ya upendo katika Ukristo na wakafanya mapendekezo yenye maana. Hivyo, natumaini nimeweza kupata ujuzi wa haki wa upendo katika Ukristo

kama ulivyo katika nadharia na kama ulivyo katika utekelezaji leo.

Mwishowe, ningependa kusema kwamba kazi hii ya sasa ilikuwa asili yake ilitungwa kama tasnifu ya shahada ya M.A. (*Religious Ethics: The contribution of Religion to Morality in Christian and Islamic Theology with Particular Reference to the Concept of Love*) na kuwasilishwa kwenye Depatment of humanities and Applied Social Studies of the Machester Metropolitan University (Idara ya ubinadamu na uchunguzi wa kijamii ya chuo kikuu cha Manchester Metropolitan) katika mwezi wa Septemba 2000. Katika toleo hili kwa faida ya wasomaji wa kawaida sura mbili juu ya mitazamo ya kimapokeo ya teolojia juu ya uhusiano kati ya dini na maadili zimeondolewa.

Wakati wa kipindi cha utafiti wangu, nimekuwa nikisaidiwa na watu wengi. Shukurani zangu zimwendee, Dr. Denis Bate, ambaye hakuwa mwema tu na msimamizi mkarimu na kiongozi wa kozi, bali vile vile ni rafiki. Kuanzia hatua za mwanzo za masomo yangu hadi mwisho, siku zote alikuwa anapatikana, alikuwa tayari kujadili na kusoma kila chembe ya kazi yangu na kila siku akinipa moyo.

Shukurani zangu vile vile Rt. Revd. Stephen Sykes na Dr. Croft kwa ukarimu wao na msaada wakati wa kukaa kwangu kwenye chuo cha st John’s College, Durham. Napenda kuelezea shukurai zangu kwa Abbot na watawa wa Ampleforth Abbey, hususan Cyprian Smith na Wulstan Petebures kwa ukarimu wao na mijadala yenye kusaidia.

Ningependa vile vile kuwashukuru wale wote ambao wamesoma na kutoa mapendekezo kwenye kazi yote au sehemu tu ya tasnifu yangu, kama vile mume wangu Dr. Mohamed Shomali, Canon Simon Hoare na Christina Hoare wa Skipton, Dimitry Bregant, Rome, Wulstan Peterburs OSB, Ampleforth.

Vile vile ni mwenye kuwiwa kwenye tasisi ya elimu na utafiti ya Imam Khomein – Qum, Iran, kwa kufadhili masomo ya mume wangu na gharama za kuishi kwetu, ambapo bila hivyo nisingeweza kukaa hapa (Uingereza) na kujifunza. Vile vile namshukuru mno mume wangu na watoto wetu wawili kwa upendo na msaada wao. Vilevile nawashukuru marafiki zangu wa Focolare, hususan

Frank Johnson kwa uaminifu wake na juhudi zake katika kuandaa kitabu hiki kwa ajili ya uchapishaji. Na mwisho lakini si haba, ningependa kutoa hisia za shukuran za dhati kwa Mungu mahala pa kila neema yake juu yetu na juu ya waja wake (neema) zilizopita na ambazo bado zipo.

**London, Machi 2001**

# Sehemu Ya Kwanza

# 1. Maadili Ya Kidini Uadilifu Unamaanisha Nini?

Kabla ya majadiliano yeyote kuhusu ‘maadili ya dini’; mtu lazima afafanue anachomaanisha mtu kwa kusema ‘maadili au ‘-a kimaadili’ kwa upande mmoja na ‘dini’ au ‘-a kidini’ kwa upande mwingine. Katika kitabu hiki sitofautishi kati ya ‘kimaadili’ na ‘uadilifu’ ingawa natambua kwamba kwa asili maneno haya mawili yanatokana na asili tofauti:[1]

Maadili huonesha watu jinsi ya kuondoa sifa mbaya kwao wenyewe na jinsi ya kukuza sifa nzuri. Mifumo tofauti ya maadili yaweza kutofautiana katika msisitizo wao. Kwa mfano, katika maadili ya kimagharibi msisitizo mkubwa (au msisitizo pekee) kwa kawaida umewekwa juu ya tabia ya mwanadamu na desturi. Na hivyo Paul Foulqilie anafafanua maadili kama mfumo wa desturi, mila ambayo huwaongoza wanadamu kwenye malengo yao.[2]

Kwa upande mwingine tunaona kwamba baadhi ya mifumo ya maadili huchukua tabia za wanadamu kwa uzito zaidi. Kwa mfano Sadr al-Din al- shirazi, mwanafalsafa Mwislamu mashuhuri, huelezea tabia za wanadamu na desturi zilizochimbukia kutoka kwenye tabia hizi kama masuala ya maudhui mbili tofauti.[3]

Ili kuelezea ni aina gani ya uchunguzi wa maadili uliohusishwa hapa wakati wa kujadili maadili ya kidini lazima nioneshe kwamba kuna aina tatu za uchunguzi wa kimaadili: maadili ya kielelezo, maadili kusanifisha na maadili uchanganuzi.

Maadili ya kielelezo ni jabarati ya uchunguzi wa mifumo ya unyofu au desturi za mtu fulani au kundi au jamii au dini au vitu kama hivyo. Kwa mfano, maadili ya kielelezo yaweza kufanya jukumu la kutupatia sisi maelezo ya uadilifu wa Socrates au Ugiriki ya kale au maadili ya Kiislamu au hata ya ki-Marx. Mbinu hapa ni kivielelezo tu ili kutoa taarifa sahihi juu ya ni nini haswa mfumo wa maadili, au mfano au desturi, na sio nini kitakachokuwa pale. Hivyo, hakuna hukumu ya kitathimini inayohitajika hapa.

Maadili kusanifisha hushughulikia nadharia za maadili juu ya usahihi wema na uovu. Hujibu maswali kama haya: Ni kitu gani kinafanya kiten- do kuwa sahihi kimaadili au makosa kimaadili? Je, kitendo ni kizuri au sahihi kama kimeleta furaha au raha, au je kitendo ni kizuri kama ni kizuri kwa chenyewe bila kujali matokeo yake? Vile vile maadili kusanifisha hujadili hadhi ya maadili ya suala makhususi kwa mfano; kutoa mimba ni kitendo kizuri au kibaya?

Maadili ya uchanganuzi hayashughuliki na jarabati au ukweli wa kihisto- ria. Wala hayashughuliki na uamuzi wa kutathimini au kusanifu. Bali huchunguza maswali kuhusu maadili kama: Nini maana au matumizi ya maneno kama vile sahihi au kosa?’ Je, maadili na uamuzi wa kutathimini waweza kuthibitishwa? Kama ndio, vipi? Nini asili ya uadilifu? Ni nini kinachomaanishwa na wakala huria au wakala mhusika?

Kihistoria, filosofia ya maadili ya uchanganuzi imejumuisha maadili ya kielelezo na ya kusanifisha. Hata

hivyo, wanafalsafa wengi wa hivi karibuni, wanatetea zaidi filosofia ya uchaganuzi, wameifanya ya pekee kwa maadili ya uchaganuzi.
Wanaamini kwamba uchunguzi wa kifilosofia unawezekana tu katika kushughulikia masuala ya maadili ya uchaganuzi. Hapa, inafaa kuangaliwa kwamba wanafalsafa wa maadili kwa kawaida huchukuwa sentensi ya maadili kuwa sentensi ambayo ina moja ya dhana saba zilizotajwa hapa chini kama kiarifu chake. Dhana hizo saba ni: wema dhidi ya ubaya, sahihi dhidi ya makosa, kupasika dhidi ya kutopaswa, na jukumu. Kwa mfano, 'kusema ukweli ni vizuri' ni sentensi ya maadili kwa sababu kiarifu chake ni moja ya dhana za maadili. Hata hivyo, 'Wema ndio unaeleta furaha kubwa kwa idadi kubwa mno ya watu' sio sentensi ya maadili, ingawa inahusiana na maadili. Kwa maneno mengine ni uchanganuzi wa maadili zaidi kuliko uadilifu.[4]

## 2. Ni Nini Kinachomaanishwa Na Dini?

Nikiwa nimefafanua kinachomaanishwa na 'maadili', sasa nitafafanua ninachomaanisha kwa 'dini' au '–a kidini'; kuna maoni tofauti kuhusiana na ufafanuzi wa dini; kwa hiyo eneo pana la madhehebu zinafikiriwa kuwa ni za 'kidini'; kwa mfano, David Edward anafafanua dini kama 'mtazamo wa heshima ya kumwogopa Mungu, au miungu au mapepo au fumbo la uhai likifuatiwa na imani na kuathiri mielekeo ya msingi ya mtu binafsi na tabia ya kikundi.[5]

Mimi binafsi sitaweza kukubaliana na ufafanuzi wa kijumla kama huu, hata hivyo, nafikiri katika utekelezaji hakuna haja ya kujisumbua sisi wenyewe kuhusu maswala ya uhusikaji wa jumla. Hapa nashughulika na dini katika muktadha mahususi.

Kwa hiyo, katika kitabu hiki kwa kusema 'dini' namaanisha tu dini zenye kumpwekesha Mungu, ukiwemo Ukristo na Uislam, na kwa 'maadili ya kidini' namaanisha kanuni za maadili, mifumo ya sheria au mifumo ya dini hizi. Uchunguzi wangu wa mifumo hii ya uadilifu utakuwa zaidi wa kivielelezo, kwa vile nitaelezea misimamo ya Uislamu au Ukiristo, au msimamo wa Waislamu binafsi au Wakiristo juu ya masuala kama vile upendo.

## 3. Sifa Bainifu Za Maadili Ya Kidini

Ilidokezwa (Markham, 1998) kwamba kuna baadhi ya nukta zinazofanana kwenye uadilifu wote wa kidini. Hapa nitaelezea nne katika hizo kama tabia za maadili ya kidini: Imani katika mapepo, utegemezi juu ya vyanzo vya kidini; imani katika kutopendelea; na athari ya ukweli wa maadili, na shughuli za kuchangiwa.

Katika dini zenye kumpwekesha Mungu, kuna asili yenye nguvu ya hali ya juu ambayo ina mamlaka juu ya wanadamu kuwaeleza mwenendo bora wa maisha na kuwaonesha jinsi ya kufikia mwenedo huo. Wafuasi wa dini yeyote ambao wana sababu fulani za kuamini katika ukweli wa dini hiyo hawatakuwa na swali kuhusu mamlaka ya chanzo hicho.

Maadili ya kidini yanaweza kufafanuliwa kama aina ya maadili ambayo hupata uhalali wake kutoka mamlaka ya kidini. Kwa hiyo mafundisho 'yaliyofunuliwa ya mamlaka hiyo yana wajibu mkubwa katika kuamua ni kipi ni sahihi au makosa. Mafundisho ya mamlaka hiyo yanaonekana katika vitabu vya dini hiyo kama Bibilia ya Wakiristo na Qur'ani ya Waislamu.

Kama ilivyo, vyanzo vya kidini kwa ajili ya maadili haviishii kwenye vitabu (maandiko). Imependekezwa (Markhamu, 1998) kwamba kunaweza kuwa na vyanzo vingine vinne ambavyo simulizi (Hadith) tofauti za kidini hutumia wakati wa kufanya maamuzi ya kimaadili.

Chanzo cha pili cha mwongozo wa kimaadili ni taasisi na desturi za kila dini. Mara nyingi hizi hufikiriwa kama nyongeza kwenye chanzo cha kwanza, yaani maandiko katika Ukiristo kwa mfano, wale walioko katka mila ya Ukatoliki wa Roma (*Roman Catholics*) wanazungumza kuhusu

Kanisa kama chombo kilichotolewa na Mungu kutafsiri maandiko kwa kila zama mpya. Kama tutakavyoona baadaye, katika Uislamu, Sunnah ni muhimu mno katika kutengeneza sheria za Kiislamu.

Chanzo cha tatu cha mwongozo wa kimaadili ni akili ya mwanadamu. Jukumu la akili katika mwongozo wa kimaadili unatakikana kujadiliwa kwa kujitegemea. Hata hivyo, kwa ufupi naweza kusema kwamba Uyahudi na Uislamu una mtazamo wa kimatumaini wa ubinadamu. Katika hali zote zawadi ya akili kwa mwanadamu ambayo, hututofautisha sisi na wanyama, ni chanzo tulichopewa na Mungu ambacho lazima kitusaidie katika kufikia kwenye uamuzi sahihi wa maadili.

Katika Ukiristo suala hili lina utata zaidi kwa kuwepo mafundisho ya dhambi ya asili. Hata hivyo desturi kubwa za Ukiristo huchangia busara kwamba ingawa dhambi imelemaza uwezo wa mwanadamu kutumia akili zao sawasawa, bado ni yenye uwezo. Hakika ni wazo hili ambalo hupelekea kwenye mafundisho ya Romani Katoliki kanuni asilia. Nadharia ya kanuni asilia hushikilia kwamba watu wote kila mahali, bila msaada wa maelezo ya ufunuo, wana uwezo kwa kiasi fulani wa kuelewa ukweli wa maadili. Kwa ajili hii watu wote wanakuwa hawana kisingizio. Kuhusiana na kanuni ya maadili asilia mtazamo ulioruhusiwa wa kanisa Romani katoliki ni kama ifuatayo:

"Mtu hushiriki katika hekima na wema wa Muumba ambaye humpa yeye ustadi juu ya vitendo vyake na uwezo wa kujitawala mwenyewe pamoja na maoni kwenye lile la kweli na la wema. Kanuni asilia huelezea chimbuko la hisia ya maadili ambayo humuwezesha mtu kumaizi kwa akili mema na maovu, ukweli na uwongo.6

Chanzo cha nne cha elimu ya maadili inadaiwa kuwa ni utaratibu wa kiasili. Ian Markham (1998) anadokeza kwamba Romani katoliki ni mila bora ijulikanayo ambayo hutumia utaratibu asilia wa ulimwengu. Anatoa rejea kutoka kwenye kitabu cha st. Thomas Aquinas (aliyemfuata Aristotle) ambaye aliamini kwamba "Mungu amejenga kwenye maumbo ya viumbe wake kanuni asilia" ambapo 'ile telos* ya kila shughuli ni madhumuni sahihi kwa ajili ya shughuli hiyo.'

Markham anatoa mfano mashuhuri wa uume, ambao kwa mujibu wa mafundisho ya Romani Katoliki una

telos* ya uzazi. Kwa hiyo ni kiyume na maumbilena hivyo utovu wa maadili – kuutumia uume kwa shughuli nyingine kama vile punyeto na ulawiti, au kuuzuia uume kutotekeleza madhumuni ya asili kwa matumizi ya dawa au vifaa vya kuzuia uzazi7

Chanzo cha tano na cha mwisho cha athari za maadili ni uzoefu wa kidini. Desturi nyingine huamini kwamba unaweza kugundua kile Mungu ana– chotaka kwa ajili yako kupitia uzoefu wa kidini na swala, ambazo wakati mwingine yaweza kuwa dhidi ya maadili yanayokubalika ya zama fulani.

Desturi zote kubwa za kidini huamini kwamba maamuzi ya kimaadili ni mambo ya ukweli na ugunduzi. Ingawa kunaweza kukawa na kutokuelewana kati ya baadhi za dini kuhusu maudhui ya uadilifu, kana kuelewana juu ya tabia ya uadilifu. Wanachukulia uadilifu kuwa yameota mizizi katika umbo la ulimwengu na nje ya mipaka ya maamuzi ya mwanadamu. Wanaamini kwamba athari za maadili huvuka uwezo wa jumuiya za wanadamu, zimechibiwa chini, kwa namna fulani ndani ya maumbo ya ulimwengu, na zenye kuwabana watu wote kila mahali.

Licha ya uchagamano wa kila dini moja, nukta zinazofanana kati ya dini zote ni kwamba zote zinachukulia fikra fulani kuwa zenye umuhimu sana kwa wanadamu wote. Sasa tutafanya rejea kwenye fikra nne kama hizo: kujifunga kwenye upendo, umuhimu wa familia, umuhimu wa ibada, na ulinzi wa maisha ya mwanadamu. Kuna ushirikiano wa uwajibikaji kwenye upendo na huruma. Ingawa sifa hizi zinajulikana katika njia tofauti ndani ya desturi tofauti, ni sifa zinazotambulika kiulimwengu. Katika sehemu mbili zifuatazo za kitabu hiki nitachunguza mitazamo ya Ukristo na Uislamu juu ya upendo.

Fikira ya pili ambayo inapatikana kwenye desturi kubwa za kidini ni umuhimu wa familia na wajibu mkamilifu wa wanaume na wanawake. Katika (mafundisho ya) dini ya Uyahudi, Ukiristo na Uislamu, Hawa (mwakilishi wa wanawake) aliumbwa kumsaidia Adamu (mwakilishi wa wanaume). Dini zote hizi imani ziwe zinaruhusu au la, huchukulia talaka kama kitu kisichofaa.

Katika dini zote hizi, ibada ina jukumu kubwa katika kumtengeneza mtu mwema. Ibada ni utaratibu ambao kwao maisha hugeuka kuwa ya kidini. Ibada huhuska kwenye vipengele vyote vya maisha pamoja na mwanzo na mwisho wa maisha.

Kalenda (ratiba) za kidini huhusisha ibada fulani kwa siku, majuma, miezi, na miaka. Saumu (kufunga) katika siku fulani tukufu ni kawaida kwa desturi nyingi za kidini. Ibada husaidia katika kuupa shime uadilifu na kuleta nidhamu ambazo humkinga mtu na maovu.

Desturi nyingi za kidini husisitiza ukuu na umuhimu wa mtu na maisha ya mwanadamu. Maisha ya mtu yanachukuliwa kuwa ni yenye thamani sana na lazima yaheshimiwe. Hii sio kusema kwamba bila kuwepo shuruti zozote zile maisha ya mtu yaweze kuchukuliwa; desturi nyingi za kidini huruhusu vita na adhabu kubwa katika mazingira fulani. Lakini maisha ya mwanadamu yanapewa hadhi maalumu katika mitazamo ya kimaadili.

Baada ya kujadili kile ambacho kwa kawaida huchukuliwa kama tabia za uadilifu wote wa kidini, sasa

nitafafanua zaidi juu ya maadili ya Ukristo na Uislamu, vyanzo vyao na baadhi ya maswali ya kimbinu kuhusiana na uvumbuzi wao.

## 4. Maadili Ya Ukiristo

Msingi wa maadili ya Ukristo uko kwenye Taurati ya Wayahudi, lakini sifa bainifu ya maadili ya Ukristo inaweza kugunduliwa kwa kuchunguza mafundisho ya Yesu katika Injili nne.[8]

Kama mambo yalivyo, lazima itajwe kwamba hakuna maelezo ya kinaganaga ya mafundisho ya maadili ya Yesu katika Injili. Preston anasema: "Injili ya nne huakisi katika njia yake yenyewe sifa bainifu za Yesu za mafundisho ya maadili. Hakuna hukumu juu ya suala lolote makhususi. Umakinifu uko juu ya changamoto kali ambayo Yesu analeta ili kukubali njia [yaani, mafundisho ya maadili yanayotokana na Taurati]."[9]

Khutba aliyoitoa juu ya mlima (Mt.5-7) ni mkusanyo (wa maandiko) unaokubalika zaidi wa mafundisho ya Yesu. Ingawa kulikuwa na taarifa nyingi za kihistoria na uchunguzi mkali wa Injili hizo, hapana shaka yoyote chanzo muhimu zaidi kwa Ukiristo leo ni Bibilia.

Kuwa na uwezo wa kuchunguza maadili ya Ukristo, mbali na uchunguzi wa msinngi wake katika ujumbe wa Yesu, lazima tuchunguze sehemu zinazotafsirika za Injili. Mkalimani wa Yesu ambaye kwamba tuna ushahidi zaidi kwake ni Mt. Paul. Anaonekana kuwa Mkiristo wa kwanza ambaye alitakiwa kueleza kuelewa kwake maadili ya Ukiristo kuhusiana na matatizo yaliyotangulizwa na makanisa.

## 5. Maadili Ya Uislamu

Kuna vyanzo viwili vikubwa vya maadili ya Kiislamu; Qu'ani na *Sunnah.* Qur'ani huchukuliwa na Waislamu kama Kitabu cha Mbiguni, kimejeng- wa kutokana na kutoka tu kwenye ufunuo wa Mungu. Waislamu huamini kwamba maana na maneno ya Qur'ani vyote hutoka kwa Mungu. Kimatendo, hakuna mgogoro mkubwa miongoni mwa Waislamu kuhusu tafsiri ya Aya hizo za Qur'ani ambazo zinahusika na uadilifu au kuhusu mfumo wa maadili wa ki-Qur'ani.

*Sunnah* yaweza kuchukuliwa kama utekelezaji wa mafundisho ya ki-Qur'ani kwenye matatizo ya maisha kama ilivyooneshwa kwa mifano katika matendo ya Mtume, misemo na uthibitisho (wa matendo au misemo ya wengine mbele yake). Kwa kawaida *Sunnah* ina maelezo zadi.

Miongoni mwa Shi'a, *Sunnah* hujumuisha *Sunnah* za Mtume Muhammad na watu wa nyumbani kwake, *Ahul-Bayt,* ambao wanachukuliwa kama warithi wa ilmu wake na wafuasi wa kazi yake kwa kuwasilisha na kuelezea mafundisho halisi ya Uislamu kama yalivyo katika njia ambayo yalifunuliwa kwake. Utajiri wa maandiko mbali mbali kutoka kwa Maimamu wa Shi'a juu ya masuala ya maadili ni ya msaada mkubwa kwao katika kufafanua misimamo ya Kiislamu juu ya masuala yaliyoelezewa ya maadili.

Kwa Shi'a na Waislamu wengine, chanzo kingine muhimu ni hoja au akili, *al-aql.* Ingawa chanzo

kikubwa kwa kusisitizia juu ya jukumu la akili ni Qur'ani yenyewe, kumekuweko na mgogoro miongoni mwa wanachuoni wa kidini wa madhehebu za Sunni kuhusu jukumu la akili na jinsi ya kufanya uwiano kati ya akili na ufunuo. Mgogoro kati ya *Ash'ariyah* na *Mu'tazilah* juu ya suala hili ni mashuhuri. Shi'a wana msimamo wa wazi kuhusiana na akili.

Kuna msemo mashuhuri miongoni mwa wanachuoni wa Shi'a, ambao mara nyingi huwa unatekelezwa kama hukumu nao ni: *Kullama hakama bihi al-'aql hakama bihi al-Shar'wa kullama hakama bihi al-Shar' hakam bihi al-aql.* Ina maana kwamba hukumu yoyote itakayofanywa kwa kutumia akili hukumu hiyo hiyo inafanywa na sheria ya kidini au *Shari'ah* na kinyume chake. Kwa hiyo, uthibitisho wa akili kuhusiana na masuala ya ibada unaweza kuchukuliwa kama uthibitisho wa kuruhusiwa kwake katika *Shariah.* Kwa mfano, kama haki kimantiki ni nzuri au sahihi halikadhalika itakuwa hivyo hivyo halali.

1. Maneno yaliyotumika hapo ni "Ethical! & Moral": Ethical Iinatokana na neno la kigiriki lenye maana ya tabia ya mtu binafsi. Moral ni neno la kilatini lenye maana ya desturi ya kijamii. Taz.Walliams 1997 uk 546. Sisi tumetafsiri neno "ethics" kama "maadili" na neno "moral" kama "Maadili" vile vile, na neno "morality" kama " uadilifu" Neno " religion" kama dini na neno "religious" kama "-a kidini!" Maneno Moral na Morality kwa Kiswahili yanaweza kuwa na maana ya "nyofu" na "unyofu" lakini kwenye tarjuma ya kitabu hiki maneno haya tumeyatumia kama "maadili na uadilifu". (Mtarjima)
2. Kama ilivyoelezwa katika Modarresi, 1997 uk. 18
3. Tazama al-Shirazi, 1378 A.H. Juz. 4 uk. 116
4. Taz. Frankena, 1973, uk. 10 na 98.
5. Edwards, 1999, uk. 745
6. Katekesimo ya Kanisa Katoliki, 1999, no. 1954
7. Taz. Markham, 1998, uk. 801-802

* Telos ni dhana ya kifilosofia yenye maana ya madhumuni au lengo.

8. Kama ilivyo, kuna tofauti kati ya Injili hizo nne. Kama Preston anavyosema, Injili ya Yohana "inaweza kuchukuliwa kama teule na maandiko yaliyokomaa ya tafakuri juu ya maudhui kubwa za Injili tatu za kwanza, iwapo mwandishi anazijua au simulizi tu za mdomo nyuma yake." Preston,1996, uk. 94.
9. Preston 1996, uk. 97.

# Sehemu Ya Pili

## 1. Nguzo Za Maadili Ya Ukristo

Maadili ya Ukristo, kama mfumo mwingine wa kimaadili, yamejengwa kwenye nemsi moja au zaidi. Katika suala la Ukristo, nemsi kwa kawaida zimeidadishwa kuwa ni saba, kwa kuamini kwamba hizi saba, wakati zikiunganishwa na upande wao mwingine wa maovu, yaani, madhambi makubwa saba, zinaweza kueleza upeo wote wa tabia ya mwanadamu. Hizo saba zina zile nyemi nne za 'asili,' ambazo zilikuwa za kawaida kwa ulimwengu wa zamani wa kipagani, na nyemi tatu za wema wa 'kiteolo- jia,' ambazo zilikuwa kwa makhususi zinahusishwa katika Ukristo. Wema wa asili unaweza kupatikana kwa juhudi za mwanadamu, lakini zile za kiteolojia hupatikana kama zawadi maalumu kutoka kwa Mungu.[1]

Nyemi ya za asili ni: uangalifu, kadiri, ujasiri, na uadilifu. Orodha hii inasemekana huenda nyuma mpaka kwa Socrates na kwa uhakika wa kuonekana katika Pilato na Aristotle. Wanamaadili wa Kikristo kama vile Augustine na Thomas Aquinas wameiona orodha hii kuwa ni yenye maana. Kwenye hizi nne, Ukristo unaongeza nyemi zile tatu za imani za kiteolojia, matumaini, na upendo.2

Hizi tatu kwa asili ziliwasishwa na Mtume Paul, ambaye hakuzitofautisha tu hizi tatu kama nyemi makhususi za Ukristo, bali alichagua upendo kama ndio mkubwa wa hizi tatu: 'Hivyo imani, matumaini na upendo hufuata hizi tatu; lakini kubwa ya hizi zote ni upendo.'
(1- Cor. 13:13)

Hivyo katika Ukristo upendo ukawa kiwango cha hukumu, na kama kuna mgogoro wa wajibat, kipaumbele lazima kitolewe kwenye upendo.3

Upendo ni muhimu mno kiasi kwamba safari yote ya kiroho au ya kimuujiza huonekana kama ya upendo. Akitoa mukhtasari wa kile alichosema katika kitabu chake kuhusu imani ya muujiza, William Johnson anaandika: [Imani ya muujiza] ni jawabu kwenye wito wa upendo; na kila hatua imenurishwa na kuongozwa na muwako hai, msisimko wa kibubusa, upendo ambao hauna kusita au kikwazo. Huu ni upendo ambao Paul anasema, ni bora kuliko zawadi yoyote ya kipaji, na hauna mipaka kwa hali yoyote. **"Huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahamili yote... upendo kamwe hauishi..." (1Cor. 13:7, 8.)** 4

## 2. Upendo Kama Msingi Kwa Maadili Ya Ukristo

**Matayo anatoa taarifa kwamba Yesu alisema, katika khutba aliyoitoa juu ya mlima, kwamba hakuja kuitengua sheria na manabii bali kuvitimiza:**

"Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana amin, nawaambia, mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yatimie. Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni. Maana nawaambia ya kwamba, haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni." (Mat. 5:17-20) Katika Luka 16:17, tunasoma:

"Lakini ni vyepesi zaidi mbingu na nchi vitoweke, kuliko itanguke nukta moja ya torati."
(Luk. 16:17)

Hivyo, wakati Yesu anachukuliwa kama mwalimu wa maadili, ni wazi kwamba alikuwa ni mrekebishaji wa mila ya Wayahudi zaidi kuliko mwanzishaji wa msngi mpya (wa sheria). Mila ya Wayahudi ina mwelekeo wa kuweka msisitizo mkubwa kulingana na waraka wa sheria; maelezo ya Yesu katika Injili humuelezea kama anayehubiri dhidi ya huu 'usahihi wa waandishi na Mafarisayo,' akitetea roho kuliko

waraka wa sheria. Yesu alikuwa tayari kupuuza wajibu wa Sabato, kama ni lazima. Alisema: **“Sabato iliwekwa kwa ajili ya mtu sio mtu kwa ajili ya Sabato.” (Mak. 2:27-28).**

Halikadhalika Paulo angeweza kula chakula kwa vyovyote, iwe ilikuwa Kosher au la, inategemea iwapo katika hali iliyokubaliwa, huadilisha kwa ajili ya wengine (1: Cor; 19:23–26).

Kama nitakavyoeleza kwa urefu baadae, Yesu alileta moyo wa sheria, ambao kwayo ‘zinatengemea sheria zote na mitume’ (cf. Mt. 22:40) kama moja ya upendo kwa Mungu na kwa jirani yake mtu. Na kwa vile kwa uwazi alikuwa hapendekezi kwamba mafundisho ya zamani ya ‘mitume’ yatupwe, hakuona haja ya kuendeleza mfumo mpana wa kimaadili.

Kwani uadilifu wa Ukristo unabakia kuwa ni suala la ufunuo na uvumbuzi. Hivyo, Ukristo kwa hakika kamwe hauvunji dhana ya uadilifu wa kiyahudi kama suala la sheria ya Mungu ya kuvumbuliwa kwa kusoma na kutafsiri maneno ya Mungu kama yalivyofunuliwa katika maandiko. Katika njia hii, inaonekana kwamba hakuna mgongano kati ya nafasi ya Yesu katika Mt. 5:17–20 na Luk. 16:17 na msisitizo wa Injili nyingine na barua za Paulo juu ya moyo wa sheria.

Kwa hiyo, nafikiri msisitizo wa Yesu juu ya upendo wa Mungu na upendo wa mtu kwa jirani wake kama amri mbili kubwa si za kuchukuliwa kama kukatalia kwa sheria na haja ya kuwa mtiifu kwayo. Hakika, kitu alichokuwa anashauri Yesu ni kwamba watu wake lazima watekeleze mahi- taji yote ya sheria, lakini wakati huo huo lazima waelewe kwamba nukta yote ya hili na njia pekee ya kupata uchamungu ni kumpenda Mungu na upendo wa mtu kwa jirani wake. Kufuata sheria lazima kufanywe na moyo wote na sio juu juu au kama ada tu. Kama Mt. Francis de Sales alivyoshauri,5 baadhi wanaamini kwamba ukamilifu hupatikana katika maisha ya kimaadili; wengine wanaamini kwamba ukamilifu hupatikana katika sala; wengine katika kuziendea Sacramenti mara kwa mara; wengine katika kutoa sadaka.

Lakini, anasema, wanajidanganya wenyewe. Ukamilifu unapatikana katika kumpenda Mungu kwa moyo wote. Mtu anayempenda Mungu kamwe hafanyi kitu cho chote dhidi ya utashi Wake (Mungu) na kamwe haachi kufanya kitu ambacho humpendeza Yeye (Mungu). Hii ndio maana Mt. Augustini alisema: “Mpende Mungu na fanya utakavyo.” Kwa hiyo, hakuna mkinzano kati ya ukubwa wa upendo na utii kwenye sheria.

Ukristo umepokea amri kubwa za uadilifu wake kutoka kwenye Agano la Kale.6 Katika Mark. 12:28–31 tunakukuta kisa muhimu sana: “Na mmojawapo wa waandishi akafika, akawasikia wakisemezana naye akatambua ya kuwa amewajibu vema, akawauliza, Katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza? Yesu akamjibu, Ya kwanza ndiyo hii, Sikia, Israil, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. Na ya pili ndiyo hii, mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi.” (Mrk. 12:28–31)

Kisa kama hicho hicho kinapatikana katika Mt. 22:34–40 na kuishia na msemo, ‘Juu ya amri hizi mbili sheria zote na mitume hutegemea.’ Katika Luk. 29:39–40 kisa hiki huishia na swali tofauti na jibu. Katika

Luk. 10:25–28 inasema kwamba: “Na tazama, mwanasheria mmoja alisimama amjaribu; akisema, Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele? Akamwambia, Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje? Akajibu akasema, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.”

Nikiwa nimeakisi juu ya dondoo hizi kutoka kwenye Injili na uhusiano wake na sehemu zinazofanana za Agano la Kale, tunaona kwamba Yesu, katika kujibu swali lilioulizwa na waandishi, alinukuu dondoo mbili tofauti kutoka kwenye maandiko ya Kiyahudi ambayo yalikuwa na uzoefu kwa wasikilizaji. Aliziweka pamoja kama pande mbili za sarafu ile ile. Alitaja amri ya upendo kwa jirani sanjari na amri ya upendo kwa Mungu kwenye kiwango cha juu sana na amri iliyo kubwa sana, amri ya kumpenda Mungu.[7]

Sehemu hizo mbili za Agano la Kale ni: “Sikiliza, Ewe Israili; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja. Nawe mpende Bwana Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. (Kmb. Torati: 6:4–5)

“Usimchukie ndugu yako mwako; ni lazima kumkemea jirani yako, wala usichukue dhambi kwa ajili yake. Usifanye kisasi, wala kuwa na kinyongo juu ya wana wa watu; bali mpende jirani yako kama nafsi yako; Mimi ndimi Bwana. (Wal. 19:17–18)

## 3. Upendo Na Dhana Husika

Baada ya kudokeza mukhtasari wa mjadala kuhusu Amri ya upendo, natu– fungue dhana za ‘upendo’ na visawe vyake. Kumekuwepo na fafanuzi tofauti zilizowasilishwa kwa ajili ya dhana ya ‘upendo.’ Kila kundi la wanafikira limesisitiza vipengele fulani vya dhana hii. Baadhi ni vya kifilosofia, kwa mfano, ufafanuzi wa upendo kama, ‘upendo wa kulingana au muungano na kile ambacho katika njia fulani hushikwa kama zenye hulka moja.[8]

Chervin katika kitabu: *Church of love* anasisitiza elementi tatu za upendo ambazo huonekana kukubalika kiujumla. Moja ni kwamba upendo ni tendo la kujitoa mwenyewe. Pendo sio tu kutoa kitu kwa mpendwa, huhitajia wewe kujitoa nafsi yako kwa mpendwa. Kwa mfano, kama kijana mwanamume anampa mke wake zawadi nyingi, lakini yeye mwenyewe akajitoa, mke atakuwa hana raha. Kipengele hiki cha upendo wa Mungu kwa ajili ya watu hujulikana kwa kuchukulia ukweli kwamba Amemtoa Mwanae wa pekee kwao.

Kwa maneno mengine, Amejitoa Mwenyewe kupitia kwa Mwanae. Juu ya kile ambacho Kanisa hufundisha kuhusu Mungu Baba, Katekisimo ya Kanisa la Uingereza inasema: “Kanisa linafundisha kwamba Mungu Baba aliniumba mimi na wanadamu wote, na kwamba katika upendo wake alimtuma Mwanae kupatanisha ulimwengu kupitia kwake.”[9]

Elementi ya pili ni kwamba upendo katu si wenye kutulia. Mpenzi hajitoi tu mwenyewe na kisha akapumzika. Badala yake, upendo huelekea kwenye urafiki wa karibu sana wa muungano ulio mkubwa

na mkubwa mno. Imedokezwa kwamba “Kwa upendo mtu huachana na nafsi yake, kama ilivyokuwa, na kufanya makazi yake pamoja na mtu mpendwa.”[10] Elementi ya tatu ni kwamba upendo unatengeneza. Upendo humfanya mpenzi kuishi katika njia ambayo humridhisha mpenziwe. Upendo wa mtu kwa Mungu humgeuza mtu kuwa muumini wa kweli.[11]

Mtu lazima aweke akilini kwamba kihistoria kumekuwa na mhamo katika Agano Jipya kutoka uelewaji wa upendo wa Kiyunani, ulioelezewa katika dhana ya Ki-Plato ya *eros,* kwenda kwenye uelewaji wa kibibilia wa upendo – *agape.* Ingawa upendo wa ashiki umekuwa mara kwa mara ukielewe- ka hasa kama matamanio ya kijinsia na hisia kali za mapenzi, mapokezi (classical) yake kidini na maana ya kifilosofia ilikuwa ni ‘upuuzaji wa nguvu za kiroho’[12] au ‘hamu ya udhanifu ya kupata ubora wa juu wa kiroho na kielimu’ (*Britannica, 1997*)*.*

Ukristo wa mwanzo ulichukulia *eros* (mungu wa upendo na matamanio ya kijinsia) kama muundo wa fahari kubwa ya ubinafsi na kujihami, kwa hiyo, Agano Jipya la Kigiriki halikutumia neno *eros* bali kwa kiasi mara chache sana neno ‘agape’. Agape lilitafsiriwa kwa Kilatini kama ‘caritas’ na hivyo likajitokeza kwenye Kiingeza kama ‘charity’ na baadye ‘upendo’. Katika Agano Jipya *agape* maana yake upendano kati ya Mungu na mtu. Neno kujuzu linakwenda mpaka kwenye upendo wa rafiki yake mtu tazama 1Yona 4:19–21: (“Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza. Mtu akisema,

Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; akisema, kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemuona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumuona. Na amri hii tumepewa na yeye, ya kwamba yeye ampendaye Mungu, ampende na ndugu yake.”) Brett anaandika: “Upendo wa Ukristo ndio kitu unachonidai kiuhalisi kwa sababu wewe ni mtu mwingine kama mimi. Kuna elementi ya msingi wa usawa iliyojiingiza; ni lazima tuwapende jirani zetu kama sisi wenyewe.”[13] (uk. 43)
Lazima ikumbukwe kwamba *agape* ilikuwa inatumika vile vile kwa maana ya ‘Sherehe za upendo’. Kipndi cha wakati wa karne ya kwanza AD, jumuiya za Kikristo zimejijenga kwenye vitengo vinavyojitegemea na walianza kujiona wenyewe kama Kanisa. Katika wakati huo walifanya aina mbli tofauti za ibada: ya kwanza, mikutano katika mtindo wa sinagogi ambao ulikuwa wazi kwa wadadasi na waumini na ilikuwa ina kusoma kutoka kwenye maandiko ya Wayahudi na ya pili, *agape,* au ‘sherehe za upendo’, kwa waumini tu. Ilikuwa ni chakula cha urafiki ambacho kwacho masikini walikaribishwa. Mtindo huu wa ibada ya pili, ilikuwa ni chakula cha jioni ambacho kwacho washiriki walishirikiana na wakati ambapo sherehe fupi, kukumbuka Chakula cha mwisho cha jioni, kufanya kumbu kumbu ya kusulubiwa msalabani.

Hii vile vile ilikuwa ni sherehe ya kutoa shukurani; jina la Kigiriki kwa ajili yake ni Eukaristi, ikiwa na maana ya ‘utoaji wa shukurani’. Chakula hiki cha wote taratibu kikawa hakiwezikani kwa vile jumuiya za Kikristo ziliongezeka na kuwa kubwa, na kwa hiyo Chakula cha Bwana kikawa kinafanyika kwenye hitimisho la sehemu ya umma ya ibada ya maandiko.

Dhana kama hiyo hiyo ni *‘charity’* (sadaka) (tarjuma ya neno la Kigiriki *agape,* vile vile lenye maana ya ‘Upendo’). Sadaka ni muundo wa hali ya juu sana wa upendo, upendano kati ya Mungu na mtu ambao

hufanywa dhahiri katika upendo usio na choyo wa marafiki zake mtu. Katika teolojia na maadili ya Kikristo, sadaka ni kitu bora na cha hali ya juu sana kilichooneshwa katika maisha, mafundisho na kufa kwa Yesu Kristo.

Juu ya fikra ya Ukristo kuhusu sadaka, Mt. Augustine anaandika: “Sadaka ni wema ambao wakati tabia zetu ziko sawa sawa kikamilifu, hutuunganisha na Mungu kwani kwazo humpenda Yeye”. Kwa kutumia ufanunuzi huu na fafanuzi nyingine kama hizi kutoka kwenye simulizi za Kikristo, wanateolojia wa karne za kati (Karne za 15–17 AD.), hususan Mt. Thomas, ameiweka sadaka ndani ya nemsi za kiteolojia (sanjari na imani na matumaini) na akabainisha jukumu lake kama ‘msingi au chimbuko’ la vyote. Ingawa mabishano ya Mageuzo ya Kanisa (kati ya karne ya 16) yalishughulika zaidi na ufafanuzi wa imani kuliko matumaini au sadaka, wanamageuzi walitambulisha upekee wa *agape* ya Mungu kwa mtu kama upendo usio stahili. Kwa hiyo, walitaka kwamba sadaka, kama upendo kwa mtu, iwe imetegemezwa sio juu ya matamanio ya lengo lake, bali juu ya mbadiliko wa maudhui yake kupitia nguvu ya *agape* ya kimungu.

Neno la Mt. Augustine kwa tathimini ya uadilifu ambayo hushawishi tabia ni *amor* (upendo). *Amor* ni nguvu ya maadili ambayo humsukuma mtu kwenye kitendo. Bidhaa zote duni ni za kutumiwa kwa njia au msaada wa kwa ajili ya bidhaa za hali ya juu; ni za hali juu tu zenye ‘kufurahiwa’ kama hatima ya mwisho ambayo kwayo moyo umewekwa. Bidhaa za hali ya juu ambazo kwazo kufaulu pekee kwa mtu hufikia ukamilifu wake, kwa (maneno ya) Mt. Agustine ni, Mungu ambaye asili Yake ni *agape*. Itakuwa mshiriki katika *agape* ya kimungu, upendo wenyewe. Mungu atajitoa Mwenyewe kwa watu, na kwa kushirikisha upendo Wake, watu watapen- dana kama Anavyowapenda wao, wakichukuwa kutoka Kwake uwezo wa kujitoa wenyewe kwa wengine.

## 4. Upendo Wa Mungu

Ni wazi kutokana na kile tulichosema mpaka sasa kwamba katika Ukristo upendo umehusishwa kwa wote; Mungu na wanadamu. Hata hivyo, kuna tofauti muhimu kati ya upendo wa Mungu na wa mwanadamu. Tofauti moja ni kwamba huu wa kwanza ni halisi, miliki, ambapo wa mwisho ni kiarifu. Sababu kwa ajili ya hilo ni ukweli kwamba Mungu ni pendo, lakini wanadamu wanaweza tu kufanya upendo. Wanaweza kupendeka na wenye kupenda, lakini ni Mungu tu pekee ndio pendo. Ukweli huu unaelezewa kwa uwazi mara mbili katika dondoo ifuatayo:

“Yeye asiyependa, hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni pendo. Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye. Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu. Wapenzi, ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana. Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote.

Tukipendana, Mungu hukaa ndani yetu, na pendo lake limekamilika ndani yetu. Katika hili tunafahamu kuwa tunakaa ndani yake, naye ndani yetu, kwa kuwa ametushirikisha Roho wake. Na sisi tumeona na

kushuhudia ya kuwa Baba amemtuma Mwana kuwa Mwokozi wa ulimwengu.

Kila akiriye ya kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, Mungu hukaa ndani yake, naye ndani ya Mungu. Nasi tumelifahamu pendo alilo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake." (I.Yoh; 4:8–16)

Imehojiwa[14] kwamba kwa vile upendo ni lengo la msingi la kuingiliana Kwake na binadamu, pamoja na kujionesha Yeye Mwenyewe, na upendo usio na kipimo na nje ya mipaka ya ulinganishaji, upendo unaweza kuchukuliwa kama sifa mahususi zaidi ya kuwepo Kwake. Upendo ni asili Yake na kwa hiyo, ni jina sahihi kwa ajili Yake. [15]

Mungu amewapenda wanadamu 'kwa upendo usio kikomo' (cf. Jer. 31:3). Mungu alikuwa wa kwanza kutupenda sisi. Tulikuwa hatupo bado, wala ulimwengu haujaumbwa bado, lakini tayari alikuwa ametupenda. Alitupenda wakati wote Yeye alikuwa Mungu na wakati wote Yeye Mwenyewe akiwa amejipenda.

Upendo wa Mungu kwa wanadamu umeoneshwa katika kuwepo kote na historia ya wanadamu: kama watu binafsi au kama jamii ya wanadamu. Upendo Wake umedhihirishwa katika uumbaji Wake wa wanadamu. Upendo Wake umedhihirishwa katika ulingano wa Agano la Sinai, katika uingiliaji Wake wote katika historia ya Israil, katika kuwepo Kwake wakati wote katikati ya watu Wake na katika kuendelea Kwake kuwakusanya tena na tena baada ya kuanguka kwao kabisa.

Mungu huwapenda wanadamu kiasi kwamba, sio tu kwamba Aliwapa vyote walivyo navyo, bali vile vile amefanyia kila kitu katika ulimwengu kwa faida yao.

Kama Mt. Augustino alivyodokeza, 'kila kitu katika ardhi au juu ya ardhi huzungumza nasi na kutushawishi sisi kumpenda Yeye, kwa sababu vyote hutuhakikishia kwamba Mungu amevifanya kwa ajili ya upendo kwetu. Hili ndilo wazo lote kwa urahisi mtu anaweza kuelewa kutoka dondoo ifuatayo ya Zaburi katika Agano la Kale:

"Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na mwana wa Adamu hata umwangalie? Bado umemfanya mdogo kuliko Mungu; Umemvika taji ya utukufu na heshima; umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; Umeviweka vitu vyote chini ya miguu yake. Kondoo, na Ng'mbe wote pia; Ndege wa angani na samaki wa baharini; Na kila kipitacho njia ya baharani." (Zab.8:4–8)

Upendo wa Mungu kwa mtu hauna kikomo juu ya viumbe wote wazuri ambao Mungu amempa mtu. Kama nilivyotaja mapema, mtazamo wa Ukristo ni kwamba upendo wa Mungu katika ubora wake umejitokeza kati– ka kujitoa Mwenyewe kupitia kwa Mwanawe. Kwa mujibu wa Mt. Yohana, "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee..."
(cf. Yoh. 3:16)

Katika Ukristo, dhana ya upendo ya ubaba wa Mungu ni wa maana sana: Upendo wa Mungu kwa

wanadamu unafananishwa na ule wa baba kwa watoto wake. Kwa mfano, katika Agano Jipya Mungu anatajwa kama, “Baba yetu uliye mbinguni…” (cf. Mt. 6:9) na kwa vile Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuomba namna hii: “Baba yetu uliye mbimguni jina lako litukuzwe…” aya hii huchukuliwa kuwa sababu nzuri ya kufikiria kwamba Mungu anaweza kuwa na anapenda kuitwa ‘Baba.’[16]

Ni Baba aliye mbinguni ambaye “…Maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, na huwanyeshea mvua wenye haki na wasio na haki.” (cf. Mt. 5:45) Upendo wa Mungu wa ubaba hujidhihirisha wenyewe kwenye nadhari Yake kwa masikini (cf. Mt. 6:32), katika kuhusika Kwake kukubwa kwa mateka na wanaoonewa (cf. Luk. 4:18,19) na hata mkutano wake na wenye dhambi, imma wakiwa wanamtafuta au (cf. Luk. 15:4–7) au kwa imani akiwangojea ili aweze kusherehekea na kwa furaha akaribishe kurudi kwao (cf. Luk. 15:11–32)

Vile vile kuna mwelekeo katika fikra ya Ukristo kulinganisha upendo wa Mungu kwa wanadamu kibinafsi au kwa pamoja kwa ule wa bwana harusi na biharusi. Graham anahoji kwamba ulinganishi kama huo umethibitishwa kwa mujibu wa maandiko na vile vile kifilosofia. Anaamini kwamba hii ni karibu mno ya maafikiano ya kidunia. Anasema:

“Bwana wetu, ikiwa katika ardhi, uliridhia kudokeza Wewe Mwenyewe uhusiano kama huo na wazo hilo limekuwa sehemu ya kaida ya Katoliki. Mtu hanabudi kukumbuka ushawishi wa wimbo wa nyimbo za Solomon juu ya lugha ya kiroho kwa ajili ya uthibitisho wa hili.”[17]

Ni muhimu kutambua kwamba hata upendo wa viumbe kwa Mungu uko moja kwa moja katika deni la Mungu. Kama anavyosema Graham, “Mambo ya awali ya ndoa kubwa kati ya mbingu na ardhi, kama itakavy- oweza kutarajiwa, ni ya Mungu peke yake. Ni sehemu ya bwanaharusi kutoa maneno (ya posa) kwanza.[18]

Juu ya vipi mtu anaweza kutekeleza jukumu lake (pamoja na kumpenda Yeye) na kushinda ushawishi wa dhambi, katekesimo ya Romani Katoliki inaelezea: “Matayarisho ya mtu kwa ajili ya kupokea baraka tayari ni kazi ya baraka.” (na. 2001) Katekisimo iliyosahihishwa ya Kanisa la Uingereza inaandika: “Naweza kufanya mambo haya tu kwa msaada wa Mungu na kwa baraka zake. Kwa baraka za Mungu nina maana kwamba Mungu Mwenyewe hutenda ndani ya Yesu Kristo ili kusamehe, kutia moyo, na kuniimarisha kwa Roho Mtakatifu.” **(Q. 26 & Q. 27).**

Kwa ujumla, mtu anaweza kusema kwamba, tofauti na upendo wetu imma kwa Mungu au kwa wanadamu wenzetu, ambao ni jibu lisilo na hisia kwa mpendwa, upendo wa Mungu ni wenye kujenga na mashughuli. Kwa Mungu sio hali ya kwamba hutambua kitu fulani kinachopendwa kwa mtu mpendwa; bali hutoa sifa zinazofaa kwenye vitu na ‘hii kwa usahihi ndio upendo Wake kwao.’ Kama Mt. Thomas Aquinas alivyosema: “Upendo wa Mungu hushawishi na kutengeneza wema ambao uko katika vitu.” Kwa hiyo, Mungu hatupendi sisi kwa sababu ameona wema fulani kwetu; ni kwa sababu anatupenda ndio tukawa na wema.

Hivyo katika upendo wa Mungu tunaona ukamilifu na msingi bora usio na ubinafsi. Hakuna kitu pale

kabla ya tendo Lake la upendo, hivyo hapati chochote kutoka kwa mpendwa, au kutoka kwenye pendo lenyewe. Mungu ana uhai wote na wema ndani yake, na kwa hiyo, hapati cho chote kwa kutupenda sisi. Haiwezekani kufikiria kwamba Anaweza kushiriki au kupata kutokona na kile ambacho tayari anacho.

Kwa kawaida swali hujitokeza; ni kwa nini Mungu aumbe ulimwengu. Kuna jibu la pamoja katika kaida ya Ukristo. Mungu aliumba mbingu na ardhi 'kuonesha ukweli Wake Mwenyewe na wema na uzuri.'[19] Tunaona katika kitabu cha Mifano kwamba, 'Bwana amefanya vitu vyote kwa ajili Yake Mwenyewe.' (Mif. Xvi, 4)[20] Graham anaongeza kwamba 'itakuwa sawa na dhambi ya mauti katika Mungu kutengeneza ulimwengu si kwa lengo lingine bali kusaidia wema mkamilifu ambao ni yeye.'[21] Anahoji kwamba ni asili ya kile ambacho ni kizuri kuwasiliana chenyewe na wengine (*Banum est diffusivum sui*). Uzoefu vile vile huelezea kwamba, kwa kawaida watu wema ni wakarimu, wasio na ubinafsi na uwezo wa kuingia kwenye mawazo na hisia za watu waliomzunguka, ambapo watu wabaya ni wachoyo, wabinafsi na wanashindwa kuanzisha urafiki na wengine na kuwa na huruma nao.

## 5. Upendo Wa Mwanadamu Kwa Mungu

Upendo ni uhusiano wa pamoja kati ya Mungu na wanadamu, na hakika, ni kwa uhusiano huu kwamba Ametuumba sisi. Tunalipa fadhila za Mungu kwetu sisi, ambazo zimedhihiri zenyewe katika neema Zake zisizo na mpaka juu yetu, angalau kwa kumpenda Yeye.

Katika dondoo, iliyojaa umaizi, Mt. Bernard anaandika: "Je, Hapaswi kupendwa kwa kulipa, wakati tunafikiri nani amependwa, Amempenda nani, na kiasi gani Alipenda? Kwani ni nani Yeye kwamba apendwe? Yule yule Ambaye kila roho hushuhudia: "Nimemwambia Bwana, Ndiwe Bwana wangu; sina wema ila utokao kwako" (Zab. 16:2 vulg). Na je, sio upendo wake ambao ni fadhila ya ajabu ambayo "…hauta- futi mambo yake…?" (1Kor. 13:5). Lakini kwa nani umedhihirishwa upendo kama huo usioelezeka? Mtume (Paulo) anatuambia: "kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake…" (Rum. 5:10). Hivyo basi alikuwa ni Mungu ambaye alitupenda sisi, ametupenda bila kizuizi, na alitupenda sisi wakati tukiwa bado ni maadui. Na ni ukubwa uliokuaje wa upendo Wake huu? Mt. Yohana anajibu: "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amuaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." (3:16)[22]

Clara Lubich, muasisi wa Facolare movement, anaandika kuhusu uwezo wa kiroho na ule wa marafiki zake: "Hadhi ambayo kwayo ametunyanyua, kwetu huonekana ni ya hali ya juu sana, na uwezekano wa kumpenda Yeye kwa kumlipa huonekana ni wa juu mno na usiostahiki kiasi kwamba tumezoea kurudia kusema: "Sio kwamba tunapaswa kusema: lazima tumpende Mungu, bali tuseme: Ee vile ambavyo tunaweza kukupenda, Bwana… vile ambavyo tunaweza kukupenda kwa moyo wetu huu mdogo"[23]

Upendo kwa Mungu hauna mpaka. Kama Mt. Bernard alivyosema: "Kipimo cha upendo Kwake ni upendo usiopimika." Sababu yenyewe ni kwamba upendo wetu kwa Mungu, Ambaye wa milele na Asiyepimika, Ambaye ametupenda sisi mwanzo na bila masilahi yoyote binafsi, hauwezi kuwa na mpaka.

Naam hakika, upendo wa mwanadamu kwa Mungu una daraja tofauti. Kama tulivyoona mapema, katika dondoo mbali mbali za Bibilia, Yesu aliomba kumpenda Bwana Mungu wako "kwa moyo wako wote, na kwa nafsi yako yote, na kwa akili yako yote, na kwa nguvu zako zote." Hili ni lengo la safari ya ki-Irifani. Upendo kwa Mungu waweza kushuhudia kufikia hatua ambayo huenea kwenye moyo wote wa mpendwa mpaka kufikia hali ambayo kwamba hajifikirii tena yeye mwenyewe au kitu kingine chochote zaidi ya Mungu.

Katika ukristo upendo kwa Mungu unaaminiwa kuwa wa wote, yaani, umetekelezwa na viumbe wote. Wakati anamuomba Mungu Mt. Augastino alionesha ukweli ule ule. Alisema: Ee Mungu, Ambaye hupendwa kwa kujua au bila kujua na kila kitu kilicho na uwezo wa kupenda."
Akielezea nukta hiyo hiyo, Graham anahoji kwamba viumbe wote, pamoja na wanadamu, hutegemea kuwepo kwao juu ya Mungu, na kwa hiyo, lazima watambuliwe kama wampendao Mungu, wakinyoosha mikono yao kimya kuelekea Kwake katika shukurani kwa kitendo Chake uumbaji."24

Kisha anaongeza kwamba kuna maana nyingine ya kumpenda Mungu, ambayo ni ya wanadamu pekee. Wanadamu wana uwezo wa kumpenda Mungu kwa kudhihirisha na kwa fahamu. Upendo huu kama ilivyo, huja baada ya ujuzi wa uainishaji wa Mungu. Tutaona katika sura ijayo kwamba kuna mtazamo mwingine ambao ni wa ma Irifani wa Kiislamu na mafilosofa ambao hukubali baadhi ya upendo wa fahamu ya Mungu katika viumbe wote, kama ilivyo, umetanguliwa na ujuzi wa uainishaji wa Mungu.

Kumpenda Mungu hakutuhitajii sisi kuacha vitu vyingine. Ni kweli kwamba ukaribu kwa Mungu katika maana hututaka sisi kujitoa kutoka kwa viumbe, wakiwemo hata sisi wenyewe, lakini hili ni kutafuta tu kwamba hakuna kinachoweza kusimama kama mshirika kwa Mungu, Mwenye kutegemewa rehema Yake. Kila kitu cha thamani kimehifadhiwa kwetu katika Mungu.

Kwa maneno mengine, "Hakuna kilicho kitukufu au cha taarifa nzuri ambacho hatimaye kitaachwa kwa ajili ya sadaka25 Katika ushuhuda wake anaelezea nukta hiyo hiyo kwa uzuri mno: "Lakini ninapenda nini, wakati ninapokupenda Wewe? Sio urembo wa miliki, sio ulinganifu maridhawa wa muda, wala ung'aavu wa mwanga, ufurshishao mno macho yetu, wala sauti tamu za nyimbo mbali mbali, wala harufu ya manukato ya maua, na lihamu, na viungo… hakuna katika hivi ninachokipenda, wakati ninapompenda Mungu wangu; na bado napenda aina ya nuru, na nyimbo, na manukato, na nyama, na kukumbatiana, wakati ninapompenda Mungu, nuru, sauti tamu, manukato, na nyama, mkumbatiano wa mtu wangu wa ndani: ambako hung'ara kwenye nafsi yangu, ni sehemu gani isiyoweza kudhibiti…Hiki ndicho nipendacho, wakati ninapompenda Mungu."
(X, Vi, 8)

## 6. Upendo Wa Mwanadamu Kwa Mwanadamu Mwenziwe

Kama nilivyotaja mapema, upendo wa mtu kwa Mungu huendelea mpaka kwa jirani, kwa wanadamu wenziwe. Upendo huu ni wa wote pamoja na wenye dhambi, wasio Wakristo na maadui. Sasa ngoja tuchunguze kwa urefu zaidi upendo kwa wenye dhambi, wasio Wakristo na maadui.

Baadhi ya misemo ya Agano Jipya (1Yoh. 4:7– 5:4) huzungumza ulazima wa upendo kwa Wakristo wenziwe. Kwa hakika, utekelezaji wa upendo wa jirani ndani ya duru ya wanafunzi (wa Yesu) ulikuwa ni wa tabia ya wazi ya Kanisa la mwanzo. Usharika wa Ukrtisto, na zaidi ya yote, vyama vidogo vidogo na madhehebu, walidumu kwa karne nyingi kwa sababu ya ukweli kwamba ndani ya jumuiya zao upendo wa jirani ulikuzwa katika hali juu sana katika muundo wa usimamizi wa kiuchungaji, ustawi wa kijamii, na msaada katika hali zote za maisha.

Hata hivyo, upendo wa Ukristo haukuishilizwa kwenye tabaka yoyote au kundi la watu. Kinyume chake, kipengele jipya katika maadili ya Ukristo ilikuwa kwamba kilivuka vikwazo vyote vya kijamii na kidini na kumuona jirani katika hali ya mwanadamu anayeteseka sana. Upendo wa kijirani lazima utekelezwe bila 'upendeleo' (James 2:9). Katika tafsir ya Luka kisa mashuhuri ambacho kwayo amri ya upendo inaelezewa, mwanasheria anamuuliza Yesu: "Ni nani jirani yangu?" katika kujibu Yesu anaelezea kisa cha Msamaria Mwema. Katika kisa hiki jirani ni mgeni, mtu asiye tegemewa (kusema kweli ni, mtu aliyepuuzwa) ambaye hahusiki na jumuiya hiyo. (Luk. 10:29–37)

Juu ya upendo wa wote, Chiara Lubich anasema: "Ni upendo ambao hujua namna ya kumkaribisha jirani aliyepotea kuridi – iwapo huyu ni rafiki, kaka, dada, au mgeni – na humsamehe mtu huyu mara idadi zisizo na kikomo.

Ni upendo ambao husherehekea zaidi juu ya mwenye dhambi ambaye hutubia kuliko juu ya watu wema elfu moja."[26] Anaongeza kwamba upendo huu "Upendo huu hauna kipimo na hautapimwa." Upendo huu "ni mwingi", "wa wote" na "wenye nguvu".

Amri ya wote ya Ukristo kwenye upendo imeelezewa kwa nguvu sana kati– ka haja yake ya mtu kuwapenda adui zake. Yesu mwenyewe anasema: "Mmesikia ya kwamba imenenwa, umpende jirani yako, na, umchukie adui yako; lakini mimi nawambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowadhi; ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio na haki." (Mt. 5:43–46) mahala pengine tunaona kwamba alisema: "Lakini nawaambia ninyi mnaosikia, Wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi, wabarikieni wale ambao wawalaani ninyi, waombeeni wale ambao wanawanea ninyi. Akupigae shavu la kushoto mgeuzie la pili, naye akunyang'anyaye joho yako, usimzuie na kanzu." (Luk. 6:27–29)

Kwa hiyo, Mkristo wa kweli huwapenda maadui zake. Hakika, kama Clement alivyodokeza,[27] kigezo cha ndani cha maendeleo ya mtu kiroho si chochote kuliko uwezo wa mtu kupenda maadui zake. Kisa kifuatacho huonesha umuhimu wa upendo (katika suala hili, upendo kwa maadui) na hali yake ya juu kwenye hofu na matumaini.

John Climcus katika kitabu chake, *The ladder of Perfection* anaandika: "Siku moja niliwaona watawa watatu wametukanwa na kudhalilishwa katika hali hiyo hiyo na wakati huo huo.

Wa kwanza alijisikia ameumizwa sana kiukatili; alihuzunika lakini aliweza kutokusema kitu chochote. Wa

pili alifurahia mwenyewe lakini alisikitika kwa ajili ya yule mtu ambaye amemtusi. Wa tatu alifikiria tu maumivu aliyopata jirani yake, na akalia kwa shauku kubwa ya huruma. Wa kwanza alisukumwa na hofu; wa pili alishawishiwa kwa matumaini ya malipo; wa tatu alisukumwa na upendo."[28]

Upendo wa mtu kwa jirani yake katika Ukristo una sifa za kufanana sana za asili, kama usawa, mwelekeo wa pamoja na ushirikiano wa asili.

Hii sifa ya usawa imeelezewa vizuri katika kile ambacho kimekwisha nukuliwa kutoka kwa Brett: "Upendo wa Ukristo ndio kitu unachoniwia kiuhalisi kwa sababu wewe ni mtu mwingine kama mimi." Kwa sababu ya elementi hii ya msingi wa usawa, maadili ya Ukristo hayategemezi kaida zake juu ya jamii, kibailojia, kisaikolojia, kifiziolojia, kiakili, au tofauti za kielimu na daraja, lakini katika ujuzi na kuwaona wanadamu kama walioumbwa katika mfano wa Mungu.

Elementi mpya ya maadili ya Ukristo ni mwanzo wa maadili ya mtu binaf- si katika maadili ya ushirika, katika kuelewa urafiki wa Wakristo kama mwili wa Kristo. Muumin binafsi hajulikani kama mtu aliyejitenga ambaye ameasisi uhusiano mpya wa kiroho na wa kiuadilifu na Mungu, bali kama 'jiwe linaloishi,' kama chembe chembe inayoishi katika mwili wa Kristo ambamo kwawo nguvu za Ufalme wa Mungu tayari zinafanya kazi.

Mt. Petro aliandika kwa wakimbizi wa Kiyahudi waliotawanyika katika Pontus, Cappadocia, Asia na Bithynia: "Mmwendee yeye, jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima. Ninyi nanyi, kama mawe yalio hai, mmejengwa mwe nyumba ya roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho zinazokubaliwa na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. (1 Pet. 2:4-5)

Na ni aina ya ushirika tunaouona katika kuelewa kwamba upendo wa Ukristo sio tu hisia za moyoni: lazima ufuatwe na matendo ya ukarimu na hatua za kumaliza mateso ya kundi lingine. Upendo sio tu kutakiana kheri au hisia za huruma. Upendo ni matendo, kutumia muda na gharama. Gilleman anasema: "Upendo wa Kristo hutwaa nafsi na mwili.
Fadhila yetu ya kiroho lazima ijipambe yenyewe katika matendo, katika kazi za ushirika za huruma (Mt. 25:35-45) na huduma za jamii (Mat. 4:32-37; 6:1).[29]

Kwa maneno mengine, Ukristo wa kiroho sio tu wa mtazamo wa ndani au mtazamo wa juu. Kama Brett anavyouelezea: "Lazima vile vile uwe wa mtazamo wa nje ukihusiana na jirani, kama ukitakiwa kuwa kamili."[30] Katika barua kwa makabila kumi na mbili yaliyotawanyika (Dispersion-Dispora), Mt. James aliandika:

"Ina faida gani, ndugu zangu, kama mtu anasema ana imani lakini haifanyi kazi, je, imani yake itamuokoa? Kama kaka au dada ni masikini na anakosa chakula cha kila siku, na mmoja wenu akasema kuwaambia 'Nendeni kwa amani, kuweni wakunjufu na maridhawa,' bila kuwapa kitu kinachohitajiwa na mwili, ina faida gani? Hivyo imani kwa yenyewe, kama haina kazi, imekufa." (James 2:14 -17)

Kwa hiyo, upendo wa Ukristo lazima uelezewe katika hali zote za mwelekeo na matendo. Matendo

lazima yawe chimbuko lake ni katika upendo, na upendo lazima uelezewe katika matendo. Uhalisi wa upendo wa Ukristo hutupeleka kwenye ubadilishanaji wa kipekee wa zawadi na mateso, ya nderemo na huzuni, ya kushindwa na ushindi; mtu binafsi ana uwezo kwa kujitolea mhanga na mateso, ili kuchangia kwenye maendeleo ya jumla. Miundo yote ya kikanisa, kisiasa na jumuiya za kijamii za Kikristo zimeasisiwa juu ya fikira hii ya msingi wa urafiki wa waumini, kama mwili wa Kristo.

Hivyo, katika Ukristo upendo una nafasi ya muhimu na jukumu zito katika teolojia na maadili. Mungu Mwenyewe ni pendo na ameumba ulimwengu kwa ajili ya upendo. Mungu ambaye ni pendo amemtuma Mwanawe kuwakomboa wanadamu na kuwalingania, akafanya ndani mfano Wake, ili kushiriki katka maisha Yake. Baba anaonesha upendo wa pekee kwa Mwana, akipitisha juu yake utukufu Wake, na Mwana anaonesha upendo wake kwa Baba kwa kutii amri Yake ili kuonesha upendo mkubwa kwa wanafunzi kwa Ufufuo wake.

Wanafunzi wanaonesha upendo wao kwa Mwana kwa kutii amri yake kupendana wenyewe kwa wenyewe, kujitoa mhanga kama Mwana mwenyewe. Kwa ujumla, jukumu la msingi la mtu ni kutekeleza upendo wa ukarimu, *agape,* na kuendeleza ufalme wa Mungu katika ardhi. Mtu lazima afanye kazi kwa ajili ya kuwepo daima kikamili- fu kwa Mungu katika ulimwengu alioufanya.

1. Kwa mujibu wa mafundisho ya Ukiristo, nems za teolojia kwa asili hazitokani na mtu wa kawaida. Hutolewa na Mungu kupitia kwa Yesu na kasha kutekelezwa na muumin. Taz. Britannica 1997.
2. Lazima ioneshwe kwamba St. Thomas katika Summa theologica anaongezea katika oradha ya nems, nems tatu za kiakili: Hekima, ujuzi na kipaji. Tazama vile vile Beirut, 1992, uk. 1992, uk. 9
3. Vicent MacNamara (1989) hushikilia kwamba kumekuwa na mabadiliko katika teolojia ya kimaadili ya Katoliki juu ya hadhi ya upendo. Huamini kwamba upendo siku zote wakati uliopita haukuwa na upekee wa daraja hili; kulikuwa na wakati ambapo upendo (au hisani) ulikuwa ukichukuliwa kama moja ya mahitaji mengi ya uadilifu.
4. Johnston, 197, uk. 135
5. MacNamara, 1987, uk. 11.
6. Mtu lazima aweke akilini kwamba, pamoja na ukweli kwamba maadili ya Ukristo chimbuko lake ni kwenye Angano la Kale na Yesu alikuwa kimsingi mtiifu kwa mila za Kiyahudi katika suala la upendo, hakuna msisitizo mwingi juu ya dhana ya upendo imma katika upande Mungu au upande wa mwanadamu katika Angano la Kale. Imedokezwa kwamba (T. Barrose, 1968, uk. 1043, 1044) Bibilia ya Kiyahudi hupendelea kutumia dhana zingine, kama vile mfungamano wa utii, uaminifu, upole na upendeleo wa nguvu ili kuelezea uhusiano wa Mungu na mtu. Kwa upande mwingine, uhusiano wa Wana wa Israil na Mungu (Yehova) huelezewa kwa dhana kama vile kuogopa, utumishi na mfungamano wa utii. Katika hali zote, ni mara chache tu upendo huongelewa. Upendo kwa mtu mwenzi kama jukumu la kidini hutokea mara tatu katika Bibilia yote ya Kiyahudi. Katika Angano Jipya upendo huwasilisha dhana kubwa kuhusu uhusianao wa Mungu na mtu. Dhana ya agano hutoa sehemu kwenye ile ya ubaba
7. Paulo alishusha sheria zote na kuishia kwenye mtu kumpenda kijarani yake, "Yule ambaye humpenda jirani yake ameitekeleza sheria....... (Rum. 13:8-10)
Kwani sheria yote imekamilishwa na neno moja.......(Wag.5:14)
8. Johann, 1967, uk. 1039
9. The revised catechism, 1996, Q. 9.
10. Graham, 1939, 22
11. Taz. Chervin,1973, 9. 10, 19, 62.
12. Johann, 1967, uk. 1040.
13. Brett, 1992, uk. 3.

14. Cerini, 1992, uk. 9

15. Barrosse (1967, uk. 1044) anafanya ulinganishi muhimu kati ya sehemu tofau- ti za N.T. yaani, Injili ya Matayo, Marko na Luka, na nyaraka za Paulo na maandiko ya Yohana. Nafikiri ulinganishi wake unaonesha kwamba kwa mfululi- zo msisitizo juu ya dhana ya upendo katika hizo sehemu tatu za N.T. huongezeka. Hufikia upeo wake katika maandiko ya Mt. Yohana ambaye kamwe hatumii neno lolote mbali na upendo kuelezea huruma za Mungu kwa mtu. Mateso ya Yesu Kristo - Kufufuka katika maandiko ya Mt. Paul huchukuliwa kudhihirisha upendo wa Yesu na wa Baba yake, ambapo katika maandiko ya Mt. Yohana huonesha kwamba Mungu ni pendo.

16. Kwa mfano, tazama Cerini, 1992, uk. 21. Lubich anaandika: "Yesu, basi hivi ndivyo unavyoionesha! Hivi ndivyo unavyotangaza ukweli kwamba nina "Baba" (Ibid), imesimuliwa kutoka C. Lubich, Diary 1964/65 (New York, 1987), uk. 72&73.

17. Graham, 1937, uk. 34

18. Graham, 1937, 36.

19. Graham, 1937, uk. 37.

20. Hii ni kweli kwa mujibu wa tarjuma ya msemo uliotajwa na Graham. Tarjuma ya kisasa inaonekana kuwa ni "Bwana ametengeneza kila kitu kwa lengo lake.

21. Graham, 1939, uk. 38

22. Berdard, 1937, Sura ya 1.

23. Lubich, May They All Be One, uk. 24. iliyodondolewa katika Cerini, uk. 38.

24. Graham, 1939,uk. 16

25. Graham, 1939, uk 60

26. C. Lubich, Meditations (London, 1989), uk. 66, 67.

27. O. Clement 1993, uk. 271.

28. Imedondolewa katika Clement, 1993, uk. 271

29. Gilleman 1967, uk. 1045.

30. Brett, 1992, uk. 3.

# Sehemu Ya Tatu

## 1. Upendo Wa Mungu Kama Sababu Kubwa Kwa Ajili Ya Uumbaji

Dhana ya upendo ni moja ya dhana muhimu katika filosofia ya Kiislamu, teolojia, irifaniyah na maadili; hakika katika baadhi ya vipengele, ina nafasi muhimu na jukumu zito. Kwa mfano, katika kufafanua mtazamo wa Kiislamu wa uhusiano kati ya Mungu na ulimwengu wote kwa ujumla, na hususan kati ya Mungu na wanadamu, upendo una nafasi muhimu zaidi.

Katika sura hii, jukumu langu kubwa ni kuelezea nafasi ya upendo katika maadili ya Kiislamu, lakini kabla ya hilo nitafafanua juu ya dhana ya upen- do katika mtazamo wa ulimwengu wote wa Kiislamu.

Mapema katika *kalam* (teolojia ya Kiislamu) mdahalo mkali ulianzishwa juu ya madhumuni ya uumbaji wa Mungu na matendo. Baadhi ya wanate- olojia wanafikiria kwamba uhusishaji wa sababu au madhumuni kwenye vitendo Vyake hutufikisha kwenye dhana kwamba Mungu ana haja na viumbe wake na Aliwaumba kukidhi baadhi ya haja, kama vile mwanadamu ambaye anasema, kufanya kazi ili kupata

pesa, au mafunzo ili kujifundisha.

Hata hivyo mtazamo wenye kuongoza, hususan miongoni mwa wale ambao wamekuwa na mwelekeo zaidi wa kimantiki, siku zote wamekuwa na mwelekeo kwamba Mungu ni Mwenye hekima (*hakim*), hivyo chochote anachofanya ni kwa ajili ya madhumuni fulani haswa ambayo yamechunguzwa kabla na kwa uangalifu. Imeelezewa katika Qur'ani kwamba: **"Je, mnafikiria kwamba tumekuumbeni bure…?" (*23:115*)**

Ama kwa hakika, ni wazi kwamba Mungu Mwenyewe hapati chochote kutoka kwa viumbe Wake, wala kwenye kitendo Chake cha uumbaji. Hii sio kwa sababu tu kwamba Yeye yuko huru kikamilifu kutokana na haja ya aina yoyote, bali vile vile kwa sababu kimantiki haiwezekani kwamba athari iliyopangwa itakuwa na aina yoyote ya ushawishi (kuhusu kuishi) juu ya sababu yake.

Chochote itakachokuwanacho athari hiyo, kimepatikana kutoka kwenye sababu. Na itakuwa ni mzunguko kuifikiria vinginevyo. Mungu hakuumba ulimwengu ili kujipatia manufaa fulani Mwenyewe, bali kutoa manufaa. Shairi mashuhuri la Kifursi linasema: "Sikuumba ulimwengu kupata manufaa fulani, Nimeumba ulimwengu kuwaonyesha watu ukarimu Wangu."

Kuna simulizi mashuhuri ya kimungu (*Hadith quds*) ambayo inaweza kupatikana katika vitabu vyote vilivyoandikwa kuhusu lengo la uumbaji katika Uislamu. Kwa mujibu wa *hadith* hii, Mwenyezi Mungu Anasema: "Nilikuwa hazina iliyofichwa; nilipenda kujulikana. Kwa hiyo niliumba ulimwengu ili kwamba niweze kujulikana."[1] Neno la asili la Kiarabu kwa neno 'upendo' limetokana na neno *hubb*, ambalo lina maana ya kutaka au kupenda.

*Hubb* ni dhana ya jumla ambayo yaweza kutumika kwenye vitu vya kawai- da, kama vile kupendelea aina fulani ya chakula, ambayo kwa Kiingereza/Kiswahili inaweza kutafsiriwa kama 'kupenda'. Au inaweza kumaanisha vitu muhimu zaidi katika uhai wa mtu, kama vile hamu kali sana ya mtu au matazamio, kwa kiasi kwamba mtu anaweza hata kuwa tayari kuangamizwa kwa ajili ya kumridhisha mpenzi au kupata matazamio yake.

*Hubb* katika hali hiyo inaweza kutafsiriwa kama 'upendo'. Kuna istilahi nyingine katika utamaduni wa Kiislamu ambayo wakati mwingine inatumika katika Kiarabu na kwa kawaida zaidi katika Kifursi kumaanisha upendo mkali, *ishq.* Vile vile kuna *wudd* urafiki mkubwa mno na yule mpendwa.

Hivyo, swali linakuja: Kwa nini Mungu kapenda kujulikana? Kwa hakika, Mungu hana tamaa ya fahari. Madhumuni ya kupenda Kwake ajulikane yanafahamika kwa kuchukulia kwamba Mungu Ni Mwenye Busara, Mwenye Huruma, na Mwenye kudra. Aliumba ulimwengu, na hususan wanadamu, ili kuwapa upeo wa huruma na ukamilifu ambao wana uwezo wa kuupokea.

Ama kwa hakika, ukamilifu wa aina yoyote ya kiumbe huamuliwa kwa daraja ya kurandana kwake au ukaribu kwa Mungu, na vipen- gele muhimu zaidi katika hili ni upendo kwa Mungu, na kabla ya hapo, kumjua Mungu, kwa vile hakuwezi kuwa na upendo bila ya kujua kina- chopendwa.

## 2. Upendo Wa Mungu Kwa Ajili Yake Mwenyewe

Kwa vile sababu ya kupenda kitu si nyingine bali ile ya ule utambuzi wa mpenzi, wa uzuri na ukamilifu, au kiujumla zaidi, uchangamfu wa mpendwa, upendo mkubwa sana uwezekanao kwa hakika ni upendo wa Mungu kwa Yeye Mwenyewe. Mungu ni mzuri zaidi na mkamilifu zaidi, na utam- buzi wake Yeye Mwenyewe vile vile ni utambuzi ulio bora, hivyo upendo Wake kwa Yeye Mwenyewe na furaha ni vitu vizito mno. Avicenna anaandika:

"Yule aliyepo kwa lazima (*wajib al-wujud*) ambaye ana ukamilifu wa juu zaidi, mbora na mwangavu na anayejitam- bua Yeye Mwenyewe kama hivyo pamoja na utambuzi mkamilifu...Yeye Mwenyewe ni mpendaji mkubwa mno na mwenye kupendwa mkubwa mno na anayo furaha kubwa mno..."[2]
Mahali pengine anasema: "Kitu ambacho kina furaha kubwa mno kuhusiana na kitu fulani ni kile cha Kwanza (*al-Awwal*) kuhusu Yeye Mwenyewe, kwa vile anao ufahamu mkubwa mno na anao ukamilifu mkubwa mno."[3]

Sadrud-din al-Shirazi, ajulikanaye kama Mulla Sadr na muasisi wa shule ya *al-Hikmah al-Muta'aliyah,* anazungumzia nukta hiyo hiyo:

"Upendo unasababishwa na kile kinachopatikana au kitakachopatikana kutoka kwa mpendwa. Wema wa hali ya juu na kuwepo na mhemuko zaidi ndio kustahiki zaidi kwa ajili ya kupendwa na upendo mkubwa mno kwa ajili ya wema. Sasa kiumbe ambacho ni huru kutokana na uwezekano na dharura, kwa ajili ya msingi wake, kina daraja ya msingi ya kupenda. Kwa hiyo, upendo kwa ajili Yake Yeye Mwenyewe ni upendo kamili zaidi na wenye utii zaidi."[4]

Aliongeza kwamba, kwa vile Mwenyezi Mungu ni halisi (sio mchanganyiko wa vitu) na sifa za Mwenyezi Mungu sio nyongeza (au kubahatisha) kwenye asili Yake katika kuwepo (fikra ambayo inakubaliwa zaidi na mafilosofa wa Kiislamu na wanateolojia wengi na hujulikana kama umoja wa asili Yake na sifa Zake), upendo Wake ni sawa sawa na asili Yake. Katika njia hii, mtu anaweza kusema kwa kuthibisha kwamba Yeye ni pendo kama ambavyo Yeye ni ujuzi na uhai.

## 3. Upendo Wa Mungu Kwa Ajili Ya Viumbe

Upendo wa Mungu kwa ulimwengu kwa ujumla, na hususan kwa wanadamu kwa pamoja unaaminiwa na kusisitizwa na Waislamu wote. Hakika, moja ya majina ya Mwenyezi Mungu ni *al-Wadud*, 'Mwenye kupenda.'

Hii ni kwa nyongeza kwenye yale majina ambayo huhusisha upendo Wake kwa vimbe, kama vile *al-Rahman* na *al-Rahim,* yenye maana ya Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu. Kila surah ya Qur'ani, isipokuwa sura ya 9, (ambayo huanza na Aya kuhusu kuwaonya makafiri) huanza kwa msemo: **"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu**".

Hata hivyo bado idadi ya kurudiwa rudi- wa kwa msemo huu katika Qur'ani ni sawa na idadi ya surah, yaani 114, kwa vile katika surah ya 27 msemo huu umtokea mara mbili. Inafaa kuta- jwa kwamba ingawa moja ya vitu vilivyohusishwa kwa Mwenyezi Mungu katika Uislamu ni ghadhabu (*ghadhad*), utekelezaji wake ni wa ukomo zaidi ukilinganisha na Huruma Yake na upendo kwa viumbe Wake. Hakika, ghadhabu Yake ni kwa wale tu ambao kwa makusudi hukufuru au hutenda vitendo viovu. Hii ni fikra ambayo Waislamu wote wanakubaliana nayo, na inaelezewa kwa uwazi katika vyanzo vingi. Hapa ningependa kutaja kauli moja yenye nguvu. Katika dua mashuhuri ya *Jushan al-Kabir*, Mwenyezi Mungu hutajwa kama 'Ambaye huruma imeitangulia (kwa kipaumbele) ghadhabu Yake'.

Kama tutakavyoona baadae, ghadhabu au hasira vile vile iko nje ya upen- do na huruma Yake. Kama upendo au huruma Yake isingekuwepo asingejali kabisa. Ni kama baba anayemkasirikia mwanawe wakati anapofanya makosa. Ni kwa sababu anajali na wasi wasi kwa ajili ya mtoto wake na kwa familia yake yote, kwa sababu anamtaka mtoto wake kurekebisha tabia yake na kuweka mfano kwa watoto wengine wasiige vitendo hivyo vya makosa.

Mwenyezi Mungu ana daraja tofauti za upendo kwa ajili ya viumbe Wake. Moja ni upendo Wake wa jumla na ulionea ambao hujumuisha viumbe wote. Kama kungelikuwa hakuna upendo kama huo kusingekuwepo na kiumbe yoyote. Upendo huu hujumuisha hata watenda maovu, kwa vile nao vile vile wanadhihirisha au kuwasilisha hatua fulani za wema katika asili yao na hiki ndicho kipengele cha uhai wao ambacho kinapendwa na Mungu, ingawa kinaweza kushindwa na kipengele cha kishetani cha tabia zao na kwa hiyo hatimaye wanaweza kuchukiwa.
Daraja kubwa ya upendo wa Mungu ni upendo Wake kwa waumini wa kweli, wale ambao wanaamini katika Yeye na kufanya matendo mema. Hao ndio watu 'Anaowapenda na ambao humpenda Yeye' (5:54). Katika Qur'ani, tunaona kwamba Mungu anawapenda 'watendao haki' (5:42; 8:60; 9:49), 'wale ambao hujitakasa wenyewe' (9:108), 'wachamungu' (3:76; 9:4 & 7), 'wale ambao hufanya wema (kwa wengine)' (5:13 & 93; 3:134 & 148; 2:195), 'wale ambao humuamini (Yeye)' (4:35), 'wavumilivu' (3:146) na 'wale ambao hutubia sana na kujitakasa wenyewe' (2:222).

Inafaa kutajwa kwamba katika Qur'ani katika masuala mengi hasira ya Mungu inaelezewa, sio kwa kuangalia katika kuchukia Kwake, bali kiasi kwa misemo ya kuzunguka, kama vile, 'Mwenyezi Mungu hampendi kila muovu afanyaye dhambi' (2:276), 'Mwenyezi Mungu hawapendi waovu' (3:57 & 140), 'hakika Mwenyezi Mungu hampendi menye fahari, ajivunaye' (4:36) na 'hakika Mwenyezi Mungu hampendi yule ambaye ni muovu, mwenye dhambi' (4:107).

## 4. Upendo Wa Mungu Kwa Ukamilifu Wa Wanadamu

Kwa mujibu wa Uislamu, daraja la juu zaidi la upendo wa Mungu kwa kiumbe yeyote ni upendo Wake kwa wanadamu wakamilifu kama vile mitume. Mtume Muhammad ana sehemu maalumu kuhusiana na hili. Moja ya vyeo vyake maarufu mno ni *Habib Ullah,* ambacho kina maana ya mpendwa wa Mungu. Katika moja ya semi mashuhuri za ki-Mungu, Mungu anamhutubia Mtume: "Lau isingekuwa wewe,

nisingeumba ulimwengu.” Kama ambavyo S.H. Nasr na wengine wengi walivyoonesha, “Mawalii wa Kiislamu kwa karne nyingi wameona katika upendo wa Mungu kwa Mtume na upendo wake (Mtume) kwa Mungu sampuli kifani ya upendo wote kati ya mtu na Muumba wake. 5

## 5. Upendo Wa Mwanadamu

Kufanana kwa kile tulichoona mwanzo katika suala la upendo wa Mungu, upendo wa mwanadamu kwa Mungu, kwa viumbe Wake, kwa matendo mema, na kwa kila moja hutekeleza jukumu zito katika mtazamo wa Kiislamu, wa kiulimwengu, hususan katika teolojia, irifani na maadili. Hakika, upendo kwa ajili ya ukweli uliounganishwa katika dini hujenga imani. Ingawa imani, kwa wanateolejia Waislamu, imeegemezwa juu ya ujuzi wa ukweli wa kidini, haipunguziki kwenye ujuzi huo. Kunaweza kuwa na watu ambao wana ujuzi mambo ya kidini, lakini ambao bado hawajitumi kwenye imani yoyote. Dini na kuamini huja tu wakati mtu kwa hiyari yake anajituma mwenyewe ukubalifu wa kanuni za imani na akawa hakatai kuzifuata. Katika maneno mengine, upendo unakuwepo tu pale wakati mtu anapopenda imani za dini na sio tu wakati mtu anapokuja kuzijua. Qur’ani inasema:

{وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنْفُسُهُمْ {14

***"Na wakazikanusha*** (***ishara za Mungu au miujiza***)***, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo..."***(*27: 14*)

Sampuli kifani ya wale ambao wanajua vizuri sana lakini wakakataa kutekeleza kile walichokwishajua ni *Iblis*, yule shetani mkubwa. Kwa mujibu wa vyanzo vya Kiislamu, *Iblis* hufanya chochote afanyacho kwa kiburi na ubinafsi, sio kwa ajili ya ujinga.

Hivyo, mtu anakuwa muaminifu na muumini wakati tu anapokuwa na heshima na upendo kwa ajili ya ukweli fulani. Tunasoma katika hadithi mashuhuri kwamba Mtume Muhammad aliwauliza masahaba wake kuhusu 'kishikizi imara cha imani'. Walipendekeza vitu tofauti kama Swala na Hijja. Wakati waliposhindwa kutoa jibu sahihi, Mtume akasema:

"Kishikizi imara cha imani ni kupenda kwa ajili ya Mungu na kuchukia kwa ajili ya Mungu, kuwa marafiki na marafiki wa Mungu na kuwakataa maadui Zake.6

Wazo kama hilo hilo limesisitizwa na Maimamu wa Nyumba ya Mtume. Kwa mfano, Fudhayl ibn Yasar, mfuasi wao, alimuuliza Imamu Sadiq iwapo upendo na chuki chimbuko lake ni imani. Imamu akajibu: "Je, imani ni kitu chochote mbali ya upendo na chuki?"7 Hadithi kama hiyo inasimuliwa kutoka kwa Imamu Baqir. Inasimuliwa vile vile kwamba Imamu Baqir alisema: "Imani ni upendo na upendo ni imani." 8

Uchunguzi wa jumla wa Qur'ani na hadithi unaonesha kwamba katika mtazamo wa Kiislamu, upendo, imma katika muundo wake Kimungu au katika muundo wa kibinadamu, ni wa vitu vya thamani na tunu

tu kwa kiasi kwamba ni vya thamani na tunu. Matokeo ni kwanza, kwamba daraja za upendo ambazo vitu tofauti hustahiki au hupokea hutofautiana kutokana na ubora wao, na pili, kwamba kila kitu ambacho kiko katika mgongano na vile vitu vyenye thamani na tunu au huzuia utambuzi wao, lazima kichukiwe.

Kwa mfano, kama haki ni yenye kupendwa, dhulma lazima ichukiwe; au kama mtu ambaye husema ukweli ni mwenye kupendwa, mtu ambaye huongopa lazima achukiwe. Kama mambo yalivyo, kuhusu vipengele vingine vya tabia zao na vitendo vyao, hali inaweza kuwa tofauti. Mtu mmoja anaweza akapendwa au kusifiwa kwa kitu fulani na wakati huo huo anaweza kuchukiwa au kulaumiwa kwa kitu kingine.

Kinyume na baadhi ya imani nyingine, kipengele kimoja cha upendo kati- ka Uislamu ni kwamba, kwa kawaida huchukuliwa sanjari pamoja na "chuki (ya maovu) kwa ajili ya Mungu." Mtu lazima apende kwa ajili ya Mungu, na kuchukia kwa ajili ya Mungu. Kuna tabia miongoni mwa baadhi ya watu kufikiri kwamba haitakikani kuwepo kwa chuki kabisa. Watu hawa hufikiria kwamba ubora na wema wa tabia na kuwa 'mkunjufu' hutegemea kuwa na urafiki na kila mtu.

Kwa hakika Uislamu hupendekeza kwa Waislamu kupenda watu na kuwa na msimamo wa kutegemea mema na huruma na uhusiano mnyofu pamoja nao, hata kama hawaamini katika Uislamu na katika Mungu. Hata hivyo sio yamkini kwa mtu ambaye ana kanuni katika maisha yake na ametoa maisha yake kufanikisha maadili matakatifu kutojali matendo maovu na uonevu wa watu waovu na kufanya urafiki na kila mtu. Hakika mtu kama huyo atapata maadui fulani. Siku zote kuna watu wazuri na wabaya katika jamii. Kuna watu wenye haki na madhalimu. Wema na ubaya ni mihimili miwili inayopingana. Kuvutiwa kwenye wema hakuwezekani bila kujitoa kutoka kwenye ubaya.

Wakti wanadamu wawili wanavutiana na wanataka kuwa marafiki, lazima tuangalie sababu kwa ajili ya hilo. Sababu si chochote bali ni mlandano na mfanano. Mpaka kuwe na mlandano baina ya watu hawa wawili, vinginevyo hawawezi kuvutiana na kuelekea kwenye urafiki wa pamoja. Rumi katika *Mathnawi* yake anataja visa viwili vizuri ambavyo huonesha ukweli huu.

Kisa kimoja ni kwamba, siku moja tabibu mwenye busara sana na mashuhuri aliwaomba wanafunzi wake wampe dawa fulani kwa ajili yake mwenyewe. Wanafunzi wake walisituka. Wakasema: "Ewe Bwana! Dawa hii ni kwa ajili ya matibabu ya vichaa, lakini wewe ni mtu mwenye busara mno ambaye tunakujua." Bwana akajibu: 'Wakati nikiwa njiani nikija hapa, nilikutana na mtu mwendawazimu. Wakati aliponiona alitabasamu. Sasa nina wasiwasi huenda ameona mfanano fulani baina yangu na yeye; vinginevyo asingefaidi vile kuniangalia."

Kisa kingine kinahusiana na mtu mwingine mwenye busara ambaye aliona aina fulani ya ndege kama kunguru amekuwa na urafiki na korongo. Walitulia pamo- ja na kuruka pamoja! Mtu yule mwenye busara hakuweza kuelewa ni kwa namna gani ndege wawili wa jamii mbili tofauti ambao pia hawana mfanano katika umbo au katika rangi wanaweza kuwa marafiki. Alikwenda karibu na kugundua kwamba wote wawili wana mguu mmoja tu.

Yule mtu mwenye busara akasema:
"Niliona urafiki baina ya kunguru na korongo.
Mshangao ulinipata, nilichunguza hali zao
Kuona ni nini dalili ya kufanana kwao ninazo weza kuziona.
Hivyo nilitambaa, na, ajabu ilyoje!
Niliona kwamba wote wawili ni vilema."

Katika Uislamu, kumekuwa na msisitizo mkubwa juu ya ulazima wa kuendeleza undugu na urafiki pamoja na watu wa imani na wenye nia njema, na wakati huo huo kupigana dhidi ya waovu. Kama mambo yalivyo, katika Uislamu upendo ni kwa wote, na Mtume wa Uislamu hakutumwa ila, **"...kuwa rehema kwa wanadamu wote" (Qur'an 21:107).**

Kwa hiyo, hata kupigana dhidi ya wale ambao hufanya maovu na dhulma ni lazima kuwe ni kwa ajili ya upendo. Ni tendo la upendo sahihi kwa ujumla na hata tuseme kumuua mtu kama Hitler, kupigana dhidi yake, kumuadhibu na ikiwa lazima kumuangamiza. Vinginevyo, atafanya uhalifu zaidi na atajishusha hadhi zaidi na zaidi na atapata adhabu kali zaidi katika ulimwengu huu na ulimwengu ujao.

Kuna kisa kizuri mno kwamba siku mmoja mtawala muonevu alimtaka mtu mchamungu kuomba kwa ajili yake. Katika kumjibu, yule mtu mchamungu alimuomba Mungu asimuache kuishi zaidi ya hapo. Yule mtawala muonevu alisituka na akasema: "Nilikuomba kuniombea mimi na sio dhidi yangu!"

Yule mchamungu akajibu: "Hivyo ndivyo nilivyofanya haswa. Ni bora zaidi kwako wewe na kwa hakika kwa ajili ya watu halikadhalika, kwamba uhai wako uwe mfupi. Utakuwa huna nafasi ya kuongeza kwenye uhalifu wako na watu watapata nafasi zaidi ya kupumzika."

Upendo wa mantiki na akili ni ule ambao unahusisha mazuri na masilahi ya binadamu na sio idadi ndogo ya watu. Mtu anaweza kufanya mambo mengi kuleta mema kwa watu au kundi ambalo huleta uovu kwa jamii au wanadamu kwa ujumla. Kwa mfano, kama hakimu akimuachia mhalifu mwenye hatia huenda amefanya kitu kizuri kwa mtu yule, lakini madhara makubwa yatakuwa yameletwa kwenye jamii na kwenye uadilifu wa haki. Mtu hatakikani aachilie upenzi wake ufiche ukweli. Kama mtoto wetu mpendwa anahitaji sindano au upasuaji haitakiwi tuuruhusu upendo wetu na mapenzi yetu yazuie kufanyika hilo.

Kwa mujibu wa Uislamu, upendo lazima uelimishwe. Upendo mtakatifu ni upendo ambao ni halisi na wenye kumaizi mno. Imekuwa ni wazo la kawaida katika mafundisho ya kimaadili ya wahubiri wakubwa wa Kiislamu na mabwana wa Kisufi kwamba mtu asiuachilie upendo wake kwa ajili ya kitu fulani au mtu fulani, umfanye apuuze ukweli wote.

Sababu ya msisitizo huu ni kwamba upendo kwa kawaida una tabia ya kumfanya mpenzi 'kipofu na kiziwi'. Kama unampenda mtu haielekei kabisa kwamba utakuwa na mtazamo wa kiupendeleo, isipokuwa kama pendo hilo limeelekezwa na akili. Hii ndio maana hata Waislamu Masufi wanajaribu wasizidiwe na upendo. Sirajud-Din anaandika:

"Sufi hana hiyari bali kuwa muangalifu, makini na mwenye kumaizi, kuweka kila kitu katika sehemu yake sahihi, na kukipa kila kitu haki yake... ni kwa sababu ya mtazamo huu kwamba Usufi ni njia ya elimu zaidi kuliko njia ya upendo. Kwani kwa hilo unaelekea kukataa upendeleo ambao mtazamo wa upendo kwa lazima huufumbia macho na hata pengine kuunga mkono."9

## 6. Upendo Wa Mwanadamu Kwa Mungu

Kwa mujibu wa Uislamu, kiwango cha chini cha mategemeo kutoka kwa waumini ni kwamba Mungu lazima awe na sehemu ya kwanza kabisa kati- ka nyoyo zao, kwa maana kwamba hakuna pendo lingine litakalopita upendo wa mtu kwa Mungu; Mungu lazima awe lengo la juu sana na mbele zaidi la upendo. Qur'a inasema:

قُلْ إِنْ كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَاكِنُ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ إِلَيْكُمْ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ {24}

***"Sema: Ikiwa baba zenu, na wana wenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyoyachuma, na biashara mnazoogo- pea kuharibika, na majumba mnayoyapenda, ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na jihadi katika njia Yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri Yake. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotovu."*** (***9:24***)

Aya hii inaonesha kwa uwazi kabisa kwamba upendo kwa Mungu lazima uwe juu kuliko chochote kile ambacho mtu anaweza kukipenda katika maisha. Ukubwa huu hujionesha wenyewe wakati upendo kwa Mungu na kwa dini Yake vikigongana na upendo kwa vitu binafsi. Katika hali hii, muumini lazima awe na uwezo wa kutoa mhanga vitu vyake binafsi avipendavyo kwa ajili ya Mungu.

Kwa mfano, kama Mungu akitutaka kutoa maisha yetu kwa ajili ya kulinda maisha ya watu wasio na hatia au usalama wa nchi yetu au vitu kama hivyo, hatupaswi kuacha mapenzi yetu ya maisha ya raha au kuwa na familia na kadhalika na kadhalika kutuzuia sisi kufanya jihadi katika njia Yake.

Kwa hiyo, muumini sio mtu anayempenda tu Mungu. Muumini ni mtu ambaye upendo kwa Mungu ni wa juu sana na anao upendo imara kabisa. Qur'ani inasema:

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَتَّخِذُ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْدَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّهِ ۖ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَشَدُّ حُبًّا لِلَّهِ ۗ وَلَوْ يَرَى الَّذِينَ ظَلَمُوا إِذْ يَرَوْنَ الْعَذَابَ أَنَّ الْقُوَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا وَأَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعَذَابِ {165}

***"Na katika watu wapo wanaochukuwa waungu wasio kuwa Mwenyezi Mungu. Wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana..."*** (***2:165***)

Kwa nini mtu ampende Mungu? Kwa mujibu wa Uislamu, sababu moja ya kumpenda Mungu ni katika ukweli kwamba Mungu ni Mwenye thamani mno, mkamilifi mno, na mzuri mno kiasi kwamba mtu hawezi kamwe kutambua, na, kwa hiyo, kwa sababu asili ya mtu hutamani uzuri na ukamilifu, humpenda Mungu.

Wanachuoni wengi wa Kiislamu, hususan wana-irfani (*mystics*), wamese- ma kwamba kila mtu huhisi katika moyo wake upendo mkubwa kwa Mungu bila ya lazima ya kuwa na habari nao. Wanahoji kwamba hata wasioamini, ambao hufukuzia tu malengo ya kiulimwengu au ya anasa, hupenda na kumuabudu Mungu katika kile wanachokichukulia kama *mwisho mzuri*. Kwa mfano, wale wanaotaka kuwa na nguvu (za kiutawala) hupenda kuwa na mamlaka ya juu sana. Kuwa Meya, au hata Rais hakutawaridhisha wao.

Hata kama wangekuwa wanamiliki ulimwengu mzima, watafikiria kuhusu kumiliki sayari nyingine. Hakuna katika ulimwengu kitakachotuliza roho zao. Mara tu watu wanapopata matlaba yao, wanatambua kwamba hayatoshelezi na hutaka wapate zaidi. Wana- irfani wa Kiislamu, kama vile Ibn Arabi, akisukumwa na Qur'ani, huami- ni kwamba sababu iliyopo nyuma ya jambo hili ni kwamba kila mtu kwa kweli anataka mwisho mzuri, yaani, Mungu. Qur'ani inasema:

{يَا أَيُّهَا الْإِنْسَانُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَىٰ رَبِّكَ كَدْحًا فَمُلَاقِيهِ {6

***"Ewe mtu! Hakika wewe unajikusuru kwa juhudi kumwendea Mola wako, basi utamkuta." (84:6)***

Hata hivyo, ukweli ni kwamba watu wengi wanafanya makosa katika kutambua ni kipi kilicho kizuri zaidi. Baadhi wanaweza kuchukulia pesa kama kitu kilicho kizuri zaidi au kwa maneno mengine, kama mungu wao. Wengine wanaweza kuchukulia nguvu za kisiasa kama mungu wao. Qur'an inasema:

{أَرَأَيْتَ مَنِ اتَّخَذَ إِلَٰهَهُ هَوَاهُ أَفَأَنْتَ تَكُونُ عَلَيْهِ وَكِيلًا {43

***"Je! Umemuona aliyeyafanya matamanio yake kuwa ndio mungu wake? Basi je, wewe utakuwa ni wakili wake?" (25:43; 45:23)***

Kama ikitokea kwamba wamefikia kile walichokipanga kama ukamilifu wao, hulka yao ya upendo kwa Mungu, uzuri wa hali ya juu, itabakia bila majibu na hivyo wataona huzuni na uvunjikaji moyo. Ibn Arabi anasema: "Hakuna kingine mbali na Mungu ambacho kimewahi kupendwa.

Mungu ndiye ambaye amejidhihirisha Mwenyewe ndani ya cho- chote kile ambacho hupendwa katika macho ya wale ambao hupenda. Hakuna kiumbe chochote isipokuwa hupenda.

Hivyo, ulimwengu wote hupenda na hupendwa, na yote haya hurejea nyuma mpaka Kwake kama ambavyo hakuna ambacho kilikuwa kinaabudiwa kingine kuliko Yeye, kwa vile chochote kile mja (wa

Mungu) alichokuwa daima akiabudu, amekuwa hivyo kwa sababu ya dhana potofu ya Mungu ndani yake; vinginevyo kamwe kisingeweza kuwa kinaabudiwa.

Mungu, Mtukufu mno, anasema (katika Qur'ani): **"Na Mola wako ameamuru usiabudu yoyote isipokuwa Yeye.**" **(17:23).** Hili halikadhalika ni suala la upendo. Hakuna mtu ambaye amewahi kupenda chochote kingine kuliko Muumba wake. Hata hivyo, Yeye, Mtukufu mno, amejificha kwao chini ya pendo kwa ajili ya Zainab, Su'ad, Hindi, Layla, dunia (ulimwengu huu), pesa, nafasi ya kijamii na vitu vyote vinavyopendwa katika ulimwengu". [10]

Ibn Arabi anaongeza kwamba: Wanairfani hawajawahi kusikia shairi lolote au sifa au kitu kama hicho bali kuhusu Yeye (na walimuona Yeye) nje ya mipaka ya mapazia.

Sababu nyingine ya kumpenda Mungu ni kulipa fadhila za upendo na baraka Zake. Kuna utajiri mkubwa wa fasihi katika vyanzo vya Kiislamu juu ya vipengele mbali mbali na vidhihirisho vya upendo wa Mungu na neema kwa wanadamu wote, ukichanganya, kwa busara, pamoja na watendao maovu na wale wasioamini katika Yeye.

Wanadamu humpenda yeyote yule awafanyiae wema, na hufurahia upendeleo na ukarimu kama huo na kujiona wenye kuwajibika kuwa wenye shukurani. Mtume alisema: "Mpende Mungu kwa sababu amefanya wema kwako na amekuteremshia neema juu yako."[11]

Kwa mujibu wa hadith za Kiislamu, Mungu aliwaambia wote; Musa na Daudi: "Nipende Mimi na nifanye Mimi nipendeke kwa watu Wangu."[12] Kisha katika kujibu swali lao la kwa vipi watamfanya Yeye apendeke kwa watu, Mungu akasema: "Wakumbusheni kuhusu neema na ukarimu wangu, kwani hawakumbuki neema Zangu bila hisia ya shukurani"[13]

Katika du'a ya kiirfani, ijulikanayo kama Mnong'ono wa mwenye kushukuru, Imamu Sajjad anasema: "Ewe Mola wangu mtiririko wa fadhila Zako zisizokatika kumenichanganya nisiweze kukushukuru Wewe!

Wingi wa neema Zako umeniacha mimi bila uwezo wa kuzihesabu sifa Zako!

Mfuatano wa matendo Yako ya upole umenipotosha kutokana na kukutaja Wewe katika kukuhimidi!

Mwendelezo wa kasi ya manufaa Yako umenizuia kueneza habari za neema Zako za uungwana!"

Kisha akaongeza:-

Ee Mola wangu, shukrani zangu zimekuwa ndogo mbele ya ukubwa wa fadhila Zako, na shukurani zangu na uenezaji wa habari umenywea kando ya ukarimu Wako kwangu!

Neema Zako zimenifunika na majoho ya nuru ya imani, na upole wa wema Wako umeweka juu yangu pazia za nguvu! Upelo Wako umenifunga na vibano visivyoweza kuondolewa na kunipamba na mikufu ya shingo ambayo haivunjiki!

Fadhila Zako ni nyingi, ulimi wangu ni dhaifu mno kuweza kuzihesabu!

Neema Zako ni nyingi, ujuzi wangu unashindwa kuzifahamu, bila ya kuzungumzia kumalika kwao!

Hivyo vipi nitapata kushukuru?14

Muumini ambaye ameanza safari yake ya kiroho kuelekea kwa Mungu, kwanza hufikia kwenye kutambua baraka za Mungu juu yake, katika ukweli kwamba Mungu humpa riziki nyingi na msaada ambao humuwezesha kutenda. Akiwa ameendelea na safari yake huku akiwa amesheheni mtazamo wa kiirfani wa ulimwengu, atatambua kwamba hakika kila kitu kizuri hutoka kwa Mungu Mwenyewe.

Tunasomaa katika Qur'ani:

{مَا أَصَابَكَ مِنْ حَسَنَةٍ فَمِنَ اللَّهِ ۖ وَمَا أَصَابَكَ مِنْ سَيِّئَةٍ فَمِنْ نَفْسِكَ ۚ} 79

***"Wema wowote uliokufikia*** (***Ewe mwanadamu***)***, umetoka kwa Mwenyezi Mungu, na ubaya wowote uliokufikia, unatoka kwako mwenyewe."*** (***4:79***)

Hakuna haja ya kufikiria vinginevyo. Sababu ya kulazimisha mateso ya kidhalimu inaweza kuwa moja ya sababu zifuatazo au mchanganyiko wa zote:

**Ukosefu wa uwezo:** Mtu ambaye huwaonea wengine anaweza kufanya hivyo kwa sababu anataka kupata kitu kutokana na uonevu huo, au kwa sababu hawezi kujizuia kufanya kitu chenye madhara kwa wengine.

**Ukosefu wa elimu:** Mtu anaweza kuwa na nia njema ya ukarimu, lakini kwa sababu ya ukosefu wa taarifa au kufanya maamuzi yenye makosa anaweza kufanya kitu ambacho humuumiza mtendewa.

**Chuki na nia mbaya:** Mtu anaweza kuwa na uwezo wa kufanya matendo mazuri na vilevile anaweza kujua jinsi ya kuyafanya, lakini anashindwa kufanya hivyo, kwa sababu sio mpole vya kutosha kufanya hivyo, au hata vibaya zaidi, kwa sababu anamchukia mtendewa na anataka kukidhi hasira na ghadhabu kwa kusababisha maumivu juu ya mtendewa.

Wanafikra wa Kiislamu wanahoji kwamba, kamwe Mungu hafanyi kitu chochote cha uovu au cha madhara kwa waja Wake, kwa vile hakuna katika sababu lizotajwa hapo juu za kuwa hivyo: Yeye ni Mwenye nguvu zote, Mwenye ujuzi wote na Mwingi wa Huruma.

Hivyo, picha ya Mungu katika Uislamu ni picha ya Yule Ambaye ni pendo, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu na Mwingi wa Ukarimu, Yule ambaye huwapenda viumbe wake zaidi kuliko vile ambavyo wangempen- da Yeye au wao wenyewe, Yule ambaye hasira na ghadhabu zake ni kutokana na upendo na hutanguliwa na upendo. Inaonekana hakuna tofau- ti miongoni mwa Waislamu katika kuamini Mungu ambaye ni pendo, ingawa wanaweza kutofautiana katika kiasi cha msisitizo ambao wanauweka juu ya

kipengele hiki cha mtazamo wa ulimwengu wa Kiislamu ukitofautisha na wengine. Kwa ujumla, inaweza ikasemwa kwamba wanairfani wa Kiislamu na Masufi wanahusika zaidi na kipengele hiki cha Uislamu kuliko mafilosofa wa Kiislamu, na kwa upande mwingine mafilosafa wanahusika zaidi kuliko wanateolejia.

Lakini, kama ilivyotajwa kabla, hakuna kutokuelewana katika kumuona Mungu kama Yule ambaye ni pendo, Mwenye Kurehemu na Mwingi wa Ukarimu. Tunasoma katika Qur'ani kwamba katika kujibu dua ya Nabii Musa kwa ajili ya maisha mazuri katika ulimwengu huu na ulimwengu ujao, Mungu alisema:

{لَ عَذَابِي أُصِيبُ بِهِ مَنْ أَشَاءُ ۖ وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ ۚ {156

***"... (Ama kwa) Adhabu yangu nitamfikishia nimtakaye, na rehema yangu imeenea kila kitu..." (7:156)***

Tunakuta katika Qur'ani kwamba kundi la Malaika ambao hubeba Arshi ya Mungu wakiomba:

وَيَسْتَغْفِرُونَ لِلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَحْمَةً وَعِلْمًا فَاغْفِرْ لِلَّذِينَ تَابُوا وَاتَّبَعُوا سَبِيلَكَ وَقِهِمْ عَذَابَ الْجَحِيمِ
7}}

***"...Ewe Mola wetu! Umekienea kila kitu kwa rehema na elimu, kwa hiyo, basi wasamehe waliotubu na wakaifuata njia yako na waepushe na adhabu ya Jahannam." (40:7)***

Ingawa pendo la Mungu sio holela na linaweza kutofautiana kutoka maudhui moja kwenda nyingine, kutokana na ubora wao, Huwapenda viumbe wote. Upendo wake kwa wafanyao makosa na wale ambao wamegeuza migongo yao Kwake ni mkumbwa mno kiasi kwamba huvuka kabisa mategemeo yao. Msisitizo juu ya kipengele hiki cha upendo wa Mungu kina sehemu kubwa ya fasihi ya Kiislamu, ikiwemo Aya za Qur'ani, *Ahadith* na mashairi. Kwa mfano, tunasoma katika Qur'ani:

قُلْ يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِنْ رَحْمَةِ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا ۚ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ
الرَّحِيمُ {53}

***"Sema: Enyi waja wangu! Mliojidhulumu wenyewe, msikate tamaa katika rehema za Mwenyezi Mungu, bila shaka Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote, hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe Mwenye kurehemu." (39:53)***

Wazo la kutubia ni moja kati ya dhana za msingi katika suala hili. Katika Aya nyingi za Qur'ani, Mungu anazungumzia uwezekano wa kutubia siku zote na kurejea Kwake, kwani Yeye ni Mwingi wa kusamehe. Anasema:

{فَمَنْ تَابَ مِنْ بَعْدِ ظُلْمِهِ وَأَصْلَحَ فَإِنَّ اللَّهَ يَتُوبُ عَلَيْهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ {39

***“Lakini mwenye kutubia baada ya dhulma yake, na akatenda wema, basi Mwenyezi Mungu atapokea toba yake, hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu.”* (*5:39*)**

Qur’ani vilevile hurejea kwenye ukweli kwamba Mungu hawasamehi tu wale ambao wanatafuta msamaha, bali vile vile Anaweza kubadilisha matendo yao mabaya kwenye kuwa matendo mema. Kwa wale ambao hutubia na kuamini na kufanya matendo mema, Qur’ani inasema: “…**Basi hao ndio ambao Mwenyezi Mungu atawabadilishia maovu yao kuwa mema, na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu.” (25:70)**

Inavutia kwamba katika Qur’ani, Mungu hawasilishwi tu kama Mwenye kukubali toba ya kweli ya waja wake na kuwasamehe wakati wakimgeukia Yeye. Hakika, ni Mungu Mwenyewe ambaye kwanza huwahudumia waja Wake ambao wamevunja, kwa njia moja au nyingine, uhusiano wao wa utumwa na Mungu, lakini bado wana upendo juu ya wema na ukweli katika nyoyo zao (yaani, nyoyo zao hazikupigwa muhuri).

Mungu huwasamehe waja kama hao na kisha wanatubia na kurejea Kwake, na kisha Mungu hugeukia kwao na kuwasamehe. Kwa hiyo, kama anavyoelezea S.H. Tabatabai mwandishi wa *Al-Mizan* kwenye tafsri ya Qur’ani katika juzuu ya 20, kila toba moja na *istighfara* ya mja mkosaji hufuatiwa na misamaha miwili ya Mungu: msamaha wa kwanza humpa mtu huyo uwezo kwa ajili ya toba ya hiyari na masamaha wa pili ni msamaha Wake (Mungu) baada ya mtu kutubia. Ukweli kwa uwazi umedokezwa na Qur’ani:

{وَظَنُّوا أَنْ لَا مَلْجَأَ مِنَ اللَّهِ إِلَّا إِلَيْهِ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ لِيَتُوبُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ {118

***“…Wakadhani kuwa hakuna pa kumkimbilia Mwenyezi Mungu ila kuelekea Kwake, kisha akawaelekea ili wapate kutubu, hakika Mwenyezi Mungu ndiye apokeaye toba, Mwenye kurehemu.”* (*9:118*)**

Kwa mujibu wa wanairfani wa Kiislamu, ujuzi wa mtu juu ya Mungu kama aliye mbora sana na mkamilifu na chanzo cha vitu vyote vizuri, na upendo wa mtu kwa Mungu Ambaye ni Pendo na Rehema, huwa imara sana na hivyo kukizunguka kile chote kitakachokaa moyoni mwa mtu. Wakati huo huo, ujuzi wa udhaifu wa mtu na kasoro mbele za Mungu huwa na nguvu sana na wa kina sana kiasi kwamba mtu atahisi hali ya utupu na kutokuwepo kitu.

Kama ambavyo mtu huyo anapoteza ubinafsi na kuwa mkarimu, atatambuliwa kwa kila aina ya uzuri. Kutoka kwenye hali ya kutokuwa na kitu, mtu hufikia daraja ya ‘hali ya kuwa na kila kitu’. Hatahisi ukomo au kizuizi. Katika hadithi mashuhuri, tunasoma kwamba “Utumwa kwa Mungu ni kiini, ambacho asili yake ni utawala”. (Shomali, 1996, uk. 32). Mtumwa halisi wa Mungu ambaye utashi wake umelingana kwenye utashi Wake ana uwezo wa kufanya matendo yasiyo ya kawaida.

Sheikh Mahmud Shabistari katika kitabu chake *Sa'adat-Nameh* ana maele- zo mazuri sana ya kile anachokichukulia kuwa ni hatua tofauti za safari ya kiroho kuelekea kwa Mungu. Anasema:

"Utumishi na ibada ya Mungu
ni imla ya Mwingi wa Huruma
kwa kila kiumbe: mtu na jinni sawa sawa.
Na bado amri yake humbana ajieleze
Mteule mno zaidi, kama Mungu alivyosema:
**"Sikuumba majinni na watu**
**ila wapate kuniabudu." (Qur'ani 51:56)**

Kupitia ibada mtu huletwa kwenye sala (maombi);
Kutoka kwenye sala mpaka kwenye fikra za kiirifani, na kisha kutoka kwenye fikra
Moto wa irifani hulipuka, mpaka aone
ukweli kwa jicho Indani la tafakari.
Hikima kama hiyo huja kutoka kwenye upendo usio na uchoyo [au upole]: Ya mwisho ni matunda yake, ya kwanza ni tawi.

Hatimaye huja upendo ambao huondosha vinginevyo vyote:
Upendo hutangua maana zote za 'mbili';
Upendo hufanya zote kitu kimoja,
Mpaka hakuna 'changu'
Wala 'chako'
Kubakia."[15]

Suhrawardi katika *The Reality of love* anafafanua mtazamo wake juu ya safari ya kiroho. Anaamini kwamba safari hii na hali zake na vituo vyake hutokeza kwenye wema (*husn*), upendo (*mihr*) na huzuni yenye tafakari (*huzn*). Anahusisha wema kwenye ujuzi wa Mungu na upendo kwenye ujuzi wa nafsi. Huzuni ni matokeo ya ujuzi wa kile kilichokuwa hakipo na kisha kikawepo.

Suhrawardi anaamini kwamba ujuzi wa nafsi huongoza kwenye uvumbuzi kwamba nafsi ni ya kimungu na hili husababisha katika kumpenda Mungu na kuwa na uzoefu wa kiirifani. Kwa hakika ni wazo la ki-Qur'ani ambalo linasisitizwa kwa uwazi na kwa wingi sana na *Sunnah* kwamba kuna ulazima wa uhusiano kati ya mtu kujua nafsi yake na kumjua Mola wake. Kwa mfano, Mtume Muhammad alisema: "Yeyote yule ambaye anaijua nafsi yake amemjua Mola wake."[16]

Suhrawardi anaamini kwamba huzuni inasababishwa na kutafakari juu ya utaratibu ambao huonesha utenganisho wa mtu na uondakaji wake kutoka kwenye makazi yake ya asili.[17]

Kwa mujibu wa Uislamu, upendo kwa Mungu ni mashughuli sana na hudhihirika wenyewe kwenye vipengele vyote vya maisha ya mtu. Hutengeneza upendo wa mtu na chuki. Vile vile hutengeneza tabia ya mtu pamoja na watu wengine na nafsi ya mtu mwenyewe. Katika hadithi mashuhuri ya *nawafil* (ibada

za suna) tunasoma: “Hakuna kinachomfanya Mja wangu kuwa karibu na Mimi kulinganisha na utekelezaji wa matendo ya wajib, wajibat.

Mja wangu daima hukaribia karibu na Mimi kwa *nawafil* mpaka nimpende. Wakati ninapompenda, basi nitakuwa masikio yake ambayo husikilizia, macho yake ambayo kwayo huonea, ulimi wake ambao kwawo huzungumzia, na mikono ambayo kwayo hushikia: kama akiniita Mimi, nitamjibu, na kama akiniomba Mimi, nitampa.”[18]

Mpenzi muaminifu hana uwezo wa kumuasi mtu mpendwa au kukataa matakwa yake. Imamu Ja’far al-Sadiq alisema: “Je, unamuasi Mungu na kujifanya unampenda? Hii ni ajabu. Kama ungekuwa mkweli ungelimtii Yeye, kwani mpendwa ni mnyenyekevu mbele ya mtu anayempenda.”[19]

Tunasoma katika Qur’ani: **“Enyi mlioamini! Atakayeiacha dini yake miongoni mwenu, basi hivi karibuni Mwenyezi Mungu ataleta watu (ambao) atawapenda, nao watampenda, wanyenyekevu kwa Waislamu, wenye nguvu juu ya makafiri, wanapigania Jihad katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawaogopi lawama za wenye kulaumu**.......**” (5: 54)**

Historia ya Uislamu imejaa kumbukumbu za wale ambao wameshirikisha upendo halisi na uliokithiri juu ya Mungu na dini Yake. Mmoja wa wale ambaye amejitoa nafsi yake kwa moyo wote kwenye Uislsmu alikuwa ni Bilal Al-Habashi, mtumwa mweusi.

Makafiri wa Makka walimtesa wakimtaka ataje majina ya masanamu yao na kuelezea imani yake kwao na kuukufuru Uislamu. Walimtesa katika jua linalochoma kwa kumlaza kwenye mawe yenye kuunguza na kuweka mawe mazito juu ya kifua chake. Abu Bakar sahaba tajiri wa Mtume, alikuwa anapita wakati aliposikia kilio cha Bilal. Alikwenda karibu na kumshauri afiche imani yake, lakini Bilal hakuwa tayari kufanya hivyo, kwa vile upendo daima ulikuwa wenye vuguvugu na wa hatari. Akielezea tukio hili, Rumi anasema:

Bilal alikuwa anautoa mwili wake kwenye miba:
Bwana wake alikuwa akimchapa viboko kwa njia ya kusahihisha,
[Akisema] “Kwanini wewe unampenda Ahmad [jina lingine la Mtume]?
Mtumwa muovu, asiyeamini katika dini yangu!”

Alikuwa akimpiga katika jua kali na miba
[Ambapo] alilia kwa kujigamba “Mmoja!”
Mpaka Siddiq [Abu Bakar] alipokuwa anapita karibu na sehemu hiyo,
Kile kilio cha “Mmoja” kiliyafikia masikio yake,
Baadae alimuona katika faragha na akamuonya:

“Ficha imani yako,
Yeye [Mungu] anajua siri [zote] zilizojificha: ifiche shauku yako.”
Yeye [Bilal] akasema: “Najuta mbele yako wewe, Ewe mwana wa Mfalme.”

Kulikua na kujuta kwingi kwa namna hii,
[Mpaka] hatimaye akaacha kujuta,
Na akatangaza na kujitoa mwili wake kwenye taabu [majonzi],
[Akilia]: “Ewe Muhammad! Ewe adui wa nadhiri na majuto!
Ee wewe ambaye umejazwa kwenye mwili na mishipa yangu yote!
Vipi kutakuwa na nafasi ndani yake ya kwa ajili ya majuto?
Kuanzia sasa nitaondosha majuto kutoka kwenye moyo huu.
Vipi nitajutia juu ya maisha ya milele?”

Upendo ndio mtulizaji wa yote, na nimetulizwa kwa upendo:
Kwa upofu wa upendo nimefanywa mnga’avu kama jua.

Ee upepo mkali, mbele Yako Wewe mimi ni bua:
Vipi nitajua wapi nitaangukia?
Iwapo mimi ni Bilal au mwezi mwandamo,
Nakimbia na kufuata mwendo wa jua Lako.
Mwezi una nini cha kufanya na unene au wembamba?
Hukimbia kwenye visigino vya jua, kama kivuli.

Wapenzi wameangukia kwenye mvo mkali:
Wameweka nyoyo zao kwenye amri ya upendo.
[Wako] kama kijaa kinachozunguka zunguka
mchana na usiku na kuomboleza kusikokwisha.[20]

## Upendo Wa Mwanadamu Kwa Wanadamu Wenzake

Muumini ambaye anampenda Mungu anategemewa kuwapenda watu Wake na kuwa na huruma kwao. Mtume alisema: “Enyi waja wa Mungu, na iwe kupenda kwenu na kuchukia kwenu kuwe ni kwa ajili ya Mungu, kwa sababu hakuna awezaye kupata wilayah (uongozi) ya Mungu bila hilo, na hakuna atakaye pata mwonjo wa imani bila hilo, ingawa swala zake na saumu zake ziwe nyingi kwa idadi.”[21]

Kama kupenda kwa mtu na kuchukia kwake ni kwa ajili ya Mungu tu, itakuwa vigumu kwake kutowapenda watu Wake. Juu ya haja ya upendo kwa watu, tunaona kwamba Qur’ani inawasifia wale watu wa nyumba ya Mtume ambao walifunga siku tatu na kutoa kila siku chakula chao kidogo amacho walikuwa nacho nyumbani siku ya kwenza kwa masikini, siku ya pili kwa yatima siku ya tatu kwa mfungwa: **“Na huwalisha chakula masikini na yatima na mfungwa hali ya kuwa wanakipenda. (Husema) Tunakulisheni kwa ajili ya radhi ya Mwenyezi Mungu tu, hatutaki kwenu malipo wala shukurani.” (76: 8-9)**

Kuna hadithi maarufu sana iliyosimuliwa katika vyanzo tofauti kwamba Mtume alisema: “Watu wote ni wa familia ya Mungu, hivyo watu wapenzi sana kwake ni wale ambao hunufaisha familia Yake zaidi.”[22]

Kwa mujibu wa hadithi, na sawa na kile kilichotajwa katika Agano jipya (Mt; 25:31-46) Siku ya Hukumu Mungu atawauliza baadhi ya watu kwa nini hawakumtembelea wakati alipokuwa mgonjwa, kwa nini hawakumpa maji wakati alipokuwa ana kiu. Watu wale watauliza: Hii imewezekana vipi kutokea ambapo Wewe ni Mola wa ulimwengu?

Kisha Mungu atawajibu: Fulani wa fulani alikuwa mgonjwa hukumtembelea na fulani wa fulani alikuwa na njaa na hukumlisha na fulani wa Fulani alikuwa na kiu na hukumpa maji ya kunywa. Je, hukujua kwamba kama ungefanya hivyo ungenikuta pamoja naye?[23]

Hivyo katika Uislamu upendo una jukumu muhimu sana katika maadili imani irifani (mafundisho ya kumfikia mungu kwa tafkira), teolojia na hata filosofia. Kuleta taswira ya Kiislamu ya ulimwengu pamoja na hadithi ya uumbwaji wa ulimwengu na binadamu na kisha utendeaji wa Mungu kwa binadamu mtu siku zote ana hitaji kuomba kwa Mungu dhana ya upendo. Mungu mwenyewe ni pendo na ameumba ulimwengu kwa upendo. Huwatendea wanadamu kwa upendo.
Imani vilevile huanza na upendo, upendo ulioshinda kabisa kwa ukweli fulani, na unatakiwa kustawishwa kwa lishe ya pendo hili mpaka kiwango cha kufikia kwamba upendo wa mtu kwa Mungu hujaza moyo wote wa mtu na ukaelekeza vipengele vyote vya maisha.

Upendo kwa Mungu unaweza kuongezeka tu wakati tunapopunguza ubinafsi wetu na kama mwishowe tunaweza kuondokana na ubinafsi tutakuwa watu wakamilifu ambao utashi na ridhaa zao zitakuwa ni utashi na radhi za Mungu.

Upendo kwa Mungu na uhuru kutokana na ubinafsi unaweza kupatikana kwanza kwa kujitolea mhanga na kuachana na matamanio yetu kwa ajili ya Mungu na watu Wake na kisha kwa kutokuwa na matamanio zaidi ya yale ambayo Mungu anayatamani na hakuna utashi zaidi kuliko wa kwake. Basi, hakika, hakutakuwa na muhanga na hakuna maumivu. Hukumu za uadilifu ni mwongozo kwenye njia hii ya upendo, ikiangazwa kuelekezwa kwa mafundisho ya wasomi na mitume.

## Hitimisho

Dini zote mbili Ukristo na Uislamu huona upendo kuwa ni dhana kubwa ya imani zao. Katika ukristo upendo ni nemsi kubwa sana (1Kor. 13:13) na amri ya upendo ni amri ya kwanza iliyo kubwa sana (Mark. 12:28-31 Mat.22:34-40, Luk. 20:25-28). Kati Uislamu 'upendo ndio kishikio madhubuti cha imani'[24] upendo ni imani. [25]

Katika dini zote upendo umehusishwa kwa Mungu na halikadhalika kwa wanadamu. Hata hivyo upendo wa Mungu ni tofauti na upendo wa mwanadamu. Upendo wa Mungu ni halisi, ni milki kwa vile Mungu Mwenyewe ni upendo.[26] Katika suala la binadamu, upendo ni kiarifu, kitu cha bahati kisichotegemewa kwao na chenye kuweza kuondolewa kutoka kwenye asili yao.

Upendo wa Mungu ni wa daima dumu. Hutupenda kwa pendo la daima na kudumu. Ameumba

ulimwengu na mwanadamu kwa upendo. Mungu anawapenda wanadamu mno sana kiasi kwamba ameumba kila kitu katika ardhi kwa ajili yao. (Katika Ukirsto kwa mfano, Zab. 8:4–8; Katika Uislamu Qur. 2: 29 & 45: 13) Katika Ukristo upendo wa Mungu kwa mara nyingi huonekana katika muundo wa uzazi. Vile vile wakati mwingine hufananishwa na upendo wa bwana harusi kwa bi harusi wake. Katika Uislamu zahania zaidi na mwelekeo wa ruiya kwa Mungu na upendo wake hutwaliwa. Upendo wa Mungu kwa mtu ni mkubwa zaidi kuliko ule wa mama au wa baba kwa mwanawe.

Kamwe Mungu haitwi baba au bwana harusi. Katika Uislamu kitu cha karibu nijuacho kwa kielezo cha ubaba na umama, na sio kile cha bwana harusi au biharusi ni kile ambacho kinaweza kuonekana katika hadithi, (na sio katika Qur'ani) kwamba watu huchukuliwa kama *'yaal'* Wake. Neno hili linaweza kutafsiriwa kama familia, lakini maana yake halisi ni kikundi cha watu ambacho mtu huchukua utunzaji wake na kwake yeye huwajibika kwa matumizi yao ya maisha. Kwa njia hii, hujumuisha wazazi wa mtu au hata wageni, kama vile yatima ambao mtu amechukuwa jukumu la kuwalipia matumizi yao Kwa hiyo Mungu hawasilishwi kama baba na watu hawawasilishwi kama watoto wake – au hata familia yake. Naam, hakika Mungu anapenda watu wote na huwaruzuku watu wote na hata wasiokuwa wanadamu kwa njia ya riziki zao.

Upendo wa Mungu una sifa ya ukamilifu na isiyo na ubinafsi na Hapati chochote kutokana na upendo wenyewe au kutoka kwa mpendwa. Mungu ameumba ulimwengu kuonesha mbele ukweli wake mwenyewe na uzuri wake.27 Amewaumba watu "ili ajulikane." 28
Katika Uislamu na Ukristo upendo kwa Mungu ni kwa wote, na hutekelezwa na viumbe wote. Kwa mfano, Mt. Augustino anasema "Ee Mungu! Ambaye hupendwa kwa kujua au bila kujua na kila kiumbe kili- cho na uwezo wa kupenda." Ibn Arabi anasema: "Hakuna chochote kama Mungu ambacho kiliwahi kupendwa."

Katika simulizi zote hizo hapo juu upendo wa mwanadamu kwa Mungu huenea mpaka kwa wanadamu wenzake. Kwa kawaida wale ambao huaminiwa kuwa karibu na Mungu hustahiki upendo zaidi. Katika Ukristo baadhi ya semi muhimu za Agano jipya (1Yoh.4:7–5:4) hufichua haja ya mtu kumpenda mkristo mwenziwe. Upendo kwa jirani huendelea mpaka kwa watu wa nje hakikadhalika. Hujumuisha hata mpaka maadui. Yesu anasema: "Bali nawaambieni, wapende maadui zako na waombee wale ambao wanakutesa ...." (Mt.5, 43–45).

Katika Uislamu sifa mashuhuri ya ki-Qura!n ya Mtume Muhammad ni "Rehema kwa walimwengu wote" *Rahmatu lil'AalimiIn*. Katika vita vya Uhud, wakati wengi wa masahaba wake, pamoja na ami yake Hamza, walipouliwa kishahidi na makafir wa kabila lake mwenyewe, na yeye alijeruhiwa na meno yake kuvunjika, Mtume alisema:

"Ewe Mola wangu! Waongoe watu wangu, Hakika hawajui" Hivyo badala ya kuwalaani aliwaombea. Mtume Muhammad alitangaza kwamba ujumbe wake ni "wakukamilisha tabia njema" Orodha ya tabia njema hujumuisha: kuwatembelea wale ambao hawakutembelei wewe, kutoa na kuwapa msaada wale ambao hawatoi au kukupa wewe msaada, kuwa muadilifu na mkarimu kwa wale ambao hawakuchunga

haki zako. Hiki ni kitu bora zaidi kuliko kulipa tu fadhila za mtu kwa mtu mwenywe.

Hata hivyo dhana ya upendo katika Uislamu imesokotana na ile ya chuki. Upendo kwa Mungu na kwa wale wema lazima uandamane na chuki kwa mwovu (shetani). Katika Uislamu imani haiwi kamili mpaka hisia na mapenzi ya mtu yote yawe yanaelekezwa na upendo kwa Mungu. Mtu wa imani hawezi kuchukia kitu au yule ambaye Mungu anampenda, kama vile ambavyo hawezi kuwapenda maadui Zake. Mungu hampendi 'muovu yeyote asiye na shukurani' (Qur'ani 9;109), 'madhalimu' (Qur'ani 3:57 & 11:40), wenye kiburi, wajivunao (Qur'ani 4:36) 'aliye haini' (Qur'ani 4:106).

Kwa njia hii, Uislamu unatofautisha kati ya kumpenda mtu na kupenda vitendo au tabia zake. Unaweza kumpenda mtu na bado ukachukia vitendo au tabia zake. Wakati mwingine upendo wako kwake huhitaji wewe kum- saidia na kumshauri na wakati mwingine hukuhitajia wewe kumzuia na ikiwa lazima kupigana naye. Hiki ndiyo kitu pekee ambacho mzazi wa kweli au rafiki mwenye upendo na mapenzi anachoweza kufanya kuhu- siana na mhalifu na muuwaji.

Hivyo kimsingi inaonekana kutokuwepo kwa kutokueleana kati ya Ukristo na Uislamu juu ya dhana ya upendo, ingawa kihistoria wakristo na Waislamu huenda walisisitiza vipengele tofauti au huenda waliutekeleza kwa namna tofauti. Ukweli unaofanana kama huo unaweza vilevile kuonekana miongoni mwa madhehebu tofauti za dini mmoja.

1. Km. Majilesi, 1983, juzuu ya 87, uk. 344.
2. Avicenna, 1956, uk. 369.
3. Avicenna, 1375 A.H., Juz. 3, uk.359.
4. Al-Shirazi, 1378 A.H., Juz. 2, uk. 274
5. Nasr, 1989,p.321
6. Al-kulayni, 1397 A.H. Kitab al- Imam wal-Kufr, "Bab al- Hubb fi Allh wal- Bughd fi Allah", no 6,p.126
7. Ibid., no.5,p.125
8. Al-Majlisi, 1983, Kitab al- Iman wal -kufr, "Bab al- Hubb fi allah wal Bughd fi Allah wal Bughd fi allah", lxvi, p.238.
9. Siraj ed-Din, 1989,p.234
10. Ibn Arabi,1994,Vol.2.,p.326
11. al-Daylami, 1370 A.H., p.226
12. al-Majlisi, 1983, Vol.8,p.351 & Vol.14,p.38; (my translation)
13. Ibid.
14. Chittick, 1987,pp.242 & 243
15. Cited from Lewisohn, 1995, pp.231 & 232
16. For a discussion on self-knowledge (ma'rifat al-nafs), See Shomali, 1996
17. For a discussion on his view in this regard see Razavi, 1997, especially p. 680
18. al-Kulayni, 1397 A.H., 'Vol. 4.' p.54
19. Cited from Mutahhari, 1985, Ch.6
20. Mathnawi, Book 1, translated by Nicholson.
21. Majlesi, 1983, Vol. 27,
22. e.g. Hemyari,1417 A.H., p. 56
23. Kwa mfano tazama: al-Hilli, 1982, p.374.
24. e.g. al-Kulayni, 1397 A.H.,p.126

25. Ibid.'p.125

26. In Christianity, e.g. 1 John 4:8-16; In Islam, it is an established idea among Muslim philosophers and many theologians regarding all Divine attributes: Go is love as He Is knowledge e.g. al-Shirazi, 1378 A.H., Vol. 2,p.274.

27. Graham, 1939,p.37

28. e.g. Majlesi, 1983, Vol.87,p.344

# Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al-Itrah Foundation:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka kumi na sita
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda

28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39. Tabia njema kwa mujibu wa Ahlul Bayt (a.s)
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya

## Back Cover

Chimbuko la chuki ni ujinga wa kutowajua wengine; Chimbuko la upendo ni ujuzi wa kuwajua wengine.

Katika kitabu hiki, mwandishi anatoa mchango muhimu sana kwenye uwelewaji wa imani mbili ambazo zimekuwa na matatizo mengi katika kujuana na kupendana kwa karne nyingi.

Katika wakati huu muhimu wa historia, wakati waumini mara kwa mara wanakaririwa na vyombo vya habari kama mashabiki wa dini, Mahnaz Heydarpoor anatuchukua nyuma kwenye kile ambacho ni muhimu katika dini zote mbili, Uislamu na Ukristo: Upendo.

Na kama alivyojihusisha yeye mwenyewe kwa kina katika mazungumzo na Wakristo, kile ambacho kimeandikwa katika kurasa hizi kimesimama si tu juu ya nadharia, bali juu matendo.

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Al-Itrah Foundation.
P. O. Box 19701,
Dar-es-Salaam, Tanzania
Simu: + 255 22 2110640 / 2127555
Email: alitrah@raha.com [14]
Website: www.ibn-tv.com [15]

---

**Source URL:** https://www.al-islam.org/fr/node/25097#comment-0

**Links**

[1] https://www.al-islam.org/fr/person/mahnaz-heydarpoor

[2] https://www.al-islam.org/fr/organization/al-itrah-foundation-0

[3] https://www.al-islam.org/printpdf/book/export/html/25097

[4] https://www.al-islam.org/printepub/book/export/html/25097

[5] https://www.al-islam.org/printmobi/book/export/html/25097

[6] https://www.al-islam.org/fr/person/dr-m-s-kanju

[7] https://www.al-islam.org/fr/taxonomy/term/2216

[8] https://www.al-islam.org/fr/tags/christianity

[9] https://www.al-islam.org/fr/tags/islam

[10] https://www.al-islam.org/fr/tags/history

[11] https://www.al-islam.org/fr/person/prophet-muhammad

[12] https://www.al-islam.org/fr/person/prophet-moses

[13] https://www.al-islam.org/fr/person/imam-jafar-al-sadiq

[14] mailto:alitrah@raha.com

[15] http://www.ibn-tv.com